Nipashe
Ijumaa Februari 7, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581945
epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital




**MWANAFUNZI** afa kwa kuangukiwa ukuta chumbani alikopanga, wenzake wajeruhiwa
UKURASA 3


UKURASA 2

**BUNGE** latoka na maazimio matano kuongeza uzalishaji sukari na mafuta



**TAKUKURU** yaibua ufisadi katika uuzaji viwanja, yaokoa mamilioni ya shilingi
UKURASA 10

# Waziri Mkuu: Tunajipanga kukabili hatua zake Trump

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akijibu maswali, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Hali inatisha Goma, siku mbili vifo kutoka 900 hadi 3,000

**WANAWAKE** wabakwa, wachomwa moto, mochwari zajaa, miili yakosa maziko... Endelea Ukurasa wa 4


UKURASA 3

## Mahakama yaagiza Dk. Slaa apelekwe kizimbani; DPP kukata rufani kupinga uamuzi wa Korti Kuu

Aliyekuwa Balozi, Dk. Wilbroad Slaa, akiwa chini ya ulinzi wa askari magereza wakati alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

**MICHEZO** YANGA YAMZAWADIA RAMOVIC USHINDI 6G UK. 24
**KATUNI** UK. 6

# Bunge laazimia mambo matano uzalishaji sukari, mafuta ya kula

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limetoa maazimio matano kuhusu uzalishaji wa sukari na mafuta ya kula nchini baada ya kubaini hautoshelezi na kusababisha kuagizwa kwa shehena za bidhaa hizo nje ya nchi.

Akiwasilisha jana bungeni taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Deodatus Mwanyika, alisema kutokana na kutopatikana kwa sukari ya kutosha kunaweza kusababisha upungufu.

Pia alisema kutowafikia watumiaji kwa wakati, kutasababisha bei kuwa juu, hivyo Bunge linaazimia serikali iendelee kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya sukari ili kuongeza uzalishaji.

Mwenyekiti huyo alisema Bunge linaazimia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) uwezeshwe kununua, kutunza na kusambaza sukari pindi uhaba unapotokea.

Pia alisema kamati inaishauri serikali kuendelea na mikakati ya kuhakikisha sukari ya kutosha inazalishwa nchini ili kupunguza kutegemea kutoka nje ya nchi na kuzalisha bidhaa zaidi ya moja, yaani sukari, umeme na 'methanol'.

"Serikali ihakikishe miundombinu ya barabara za mashambani na ya umwagiliaji katika mashamba ya miwa ya wakulima wadogo inatengenezwa ili kurahisisha usafirishaji. Pia kamati inashauri uwekezaji ufanyike ili uzalishaji wa sukari ya viwandani ufanyike hapa nchini," alisema.

Kuhusu hali ya mafuta ya kula nchini, Mwanyika alisema bado kuna upungufu unaosababishwa na wakulima wengi kusitisha kilimo cha alizeti kutokana na kukosa soko la uhakika.

Alisema upungufu huo unasababisha wafanyabiashara kuingiza shehena kutoka nje ambayo huuzwa kwa bei ya juu.

"Bunge linaazimia serikali iendelee kuhamasisha, kuendeleza na kujenga viwanda vya kutosha vya kuzalisha mafuta ya kula nchini ili kupunguza utegemezi wa uingizaji wa mafuta ya kula na kujihakikishia usalama wa chakula nchini," alisema.

Pia alisema Bunge linaazimia serikali iendelee kupitia upya vivutio ilivyotoa kwa wazalishaji wa ndani wa mafuta ili kuondoa athari zilizojitokeza kwa wakulima wa alizeti.

Kadhalika, alisema alizeti kama ilivyo kwa mazao mengine, iwekewe bei ambazo zitawavutia wakulima kuhamasika kulima kwa wingi.

Kuhusu tasnia ya chai, Bunge limeazimia serikali ikamilishe haraka majadiliano na wawekezaji wa viwanda ambao wameshindwa kuendesha mashamba na viwanda kwa lengo la kuwapa wawekezaji wengine wenye uwezo.

Aidha, alisema serikali ipitie upya mfumo wa uendeshaji wa mashamba na viwanda hivyo kwa nia ya kuwahusisha wakulima wadogo na wa kati kwenye uendeshaji na umiliki.

Katika hatua nyingine, Mwanyika alisema kamati haijaridhishwa na mchakato wa uanzishwaji wa mamlaka za usimamizi wa shughuli za maendeleo za sekta ya mifugo pamoja na sekta ya uvuvi.

Aliitaka serikali kuona umuhimu wa kukamilisha sehemu iliyobaki ili mamlaka hizi zianzishwe kutekeleza majukumu yake na kupata tija iliyokusudiwa kwenye sekta husika.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Patrobas Katambi (katikati), akizungumza na kinamama kutoka Mkoa wa Singida waliotembelea Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Mkuu: Tunajipanga kukabili hatua za Trump

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametoa msimamo wa serikali baada ya mabadiliko makubwa ambayo Serikali ya Marekani imefanya katika sera yake ya mambo ya nje, Tanzania ikijielekeza kujiimarisha na kuwa na uwezo wa ndani.

Amesema ni muhimu pamoja na upana wa uhusiano ambao wamewekeka, kuhakikisha wanajiimarisha na kuwa na uwezo wa ndani na hawaendelei kuwa tegemezi.

Majaliwa alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole akiyetaka kujua serikali inajipanga vipi na mabadiliko ya Sera za Nje ya Nchi ya Marekani ambao tangu Rais Donald Trump aingie madarakani, wamefanya mabadiliko makubwa kuhusu sera hiyo.

Mbunge huyo aliuliza mabadiliko hayo yanakwenda kuathiri vipi utekelezaji sera Tanzania kwenye elimu, afya na kiuchumi ikiwamo miradi inayofadhiliwa na USAID, PP4R na programu ya kupunguza makali ya VVU/UKIMWI.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema ni kweli serikali inaheshimu sera ya mambo ya nje na kutekeleza mikataba kama ambavyo walivyokubaliana na nchi husika.

Waziri Mkuu alisema wameanza kuona nchi zenye uwezo mkubwa, ikiwamo Marekani, zikibadilisha sera zao na kuathiri baadhi ya nchi na hata Tanzania inaweza kuzipata.

"Kwetu sisi ni muhimu kuzingatia sera za nje kama tulivyokubaliana. Ninampongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kufanya nchi hii kuwa na uhusiano na nchi nyingi duniani, Marekani ikiwa mojawapo.

"Muhimu kwetu sisi pamoja na upana huu wa uhusiano ambao tumeuweka, ni kuhakikisha kwamba tunajiimarisha na kuwa na uwezo wa ndani kwa kuhakikisha kwamba hatuendelei kuwa tegemezi.

"Lazima tujiimarishe kwenye mipango yetu, bajeti zetu ziweze kumudu na kutekeleza maeneo yote muhimu ikiwamo hiyo sekta ya afya, elimu maji na maeneo mengine kadri tulivyokubaliana na nchi husika," alisema.

Majaliwa alisema kama nchi, wana uwezo na zipo maliasili na rasilimali, kazi ambayo wanayo ni Watanzania kuhakikisha wanazitumia kujenga uchumi wa ndani na kuwezesha bajeti kutekeleza hayo.

"Marekani wameshatangaza, inawezekana na nchi nyingine ikatangaza kukawa na mabadiliko. Na sisi tunaendelea kujiimarisha kuhakikisha tunakuza uchumi wetu kupitia vyanzo vya fedha na mapato tunayaweka pamoja na kuyaingiza bungeni ili yapangiwe mpango kazi ili maeneo yaliyopungua tuweze kuyajazia," alisema.

Waziri Mkuu alisema huo ndio mkakati ambao sasa wako nao na ndivyo ambavyo wanajipanga kutokana na mabadiliko ambayo yanaendelea kwenye nchi zilizoendelea dhidi ya nchi ambazo zinaendelea kama Tanzania.

Hatua ya Rais Trump kutia saini agizo la kuiondoa nchi hiyo katika Shirika la Afya Duniani (WHO) siku chache zilizopita, tayari imetajwa kuanza kuleta athari kadhaa, hususan barani Afrika kama ilivyotarajiwa.

Licha ya kuwa kuna sheria zinazohitajika kufuatwa kwa taifa linalotaka kundoa ufadhili wake, utawala wa kiongozi huyo mpya tayari umechukua hatua ya kusitisha usambazaji dawa za kuzuia makali ya VVU, malaria na kifua kikuu (TB).

Athari hizo zinatokana na Marekani kuwa mchangiaji mkubwa wa kifedha wa WHO na programu mbalimbali zilizopo chini ya shirika hilo na taasisi nyingine kubwa za kiafya duniani.

Jumanne ya juma hili, makandarasi na washirika wanaofanya kazi na Shirika la Misaada la Marekani (USAID) nchini Tanzania na Kenya walianza kupokea barua hizo za kusitisha ufadhili huo mara moja, kulingana na vyanzo.

Hatua hiyo ni sehemu ya kusitishwa kwa misaada kwa Marekani na ufadhili uliowekwa tangu Trump aingie madarakani Januari 20, huku programu zikikaguliwa.

Ofisa Mkuu wa Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Barani Africa (CDC) Ngashi Ng'ongo amenukuliwa na shirika la habari la Reuters akisema nchi nyingi zimekuwa zinategemea uwekezaji wa Marekani kupitia WHO kufadhili shughuli za afya ya umma.

Kenya na Tanzania tayari USAID imetangaza kupunguza au kufuta shughuli kadhaa katika programu zake. Shirika hilo lilisema kuwa linakatiza huduma zote zilizokuwa zikitolewa na USAID kufuatia agizo la Rais Trump la kuondoa nchi hiyo WHO.

# Mwanafunzi afariki dunia kuangukiwa na ukuta, wenzake watatu wajeruhiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Choma, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, amefariki dunia kwa kuangukiwa na ukuta wa nyumba aliyokuwa amepanga kutokana na mvua iliyonyesha saa saba usiku huku wenzake watatu wakijeruhiwa.

Mkuu wa Shule hiyo, Lucy Kibela alitoa taarifa hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu juu ya tukio hilo, akisema nyumba nyingi ambazo wanafunzi wamepanga mitaani na vijijini si imara na zimejengwa kwa matofali ya udongo. Zinapoloa zinaanguka.

Alisema tukio hilo lilitokea saa saba Februari 5 mwaka huu, wanafunzi wanne walikuwa wamepanga katika chumba kimoja kwenye moja ya nyumba iliyoko jirani na shule hiyo.

Lucy alitaja mwanafunzi aliyefariki dunia kuwa ni Pendo Williamu (16) aliyekuwa akisoma kidato cha tatu na kwa majeruhi ni Sharida Shija (15) wa kidato cha kwanza, Neema Shija (16) wa kidato cha tatu na Regina Eliasi (16) wa kidato cha tatu.

"Wanafunzi watatu waliojeruhiwa na hali zao zinaendelea vyema na wameruhusiwa kurejea shuleni na niko nao, hali zao zikibadilika nitahakikisha wanawarejeshwa hospitalini. Suluhisho la janga hili ni kukamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi," alisema Mwalimu Lucy.

Alisema wazazi wengi wamewapangisha watoto wao mitaani jirani na shule kwa kuwa wengi wanatoka vijiji vya mbali ambako njiani wamekuwa wanakutana na changamoto mbalimbali, ukiwamo ubakaji na hivyo ili kuondoa adha hiyo, kuna haja kukamilisha ujenzi wa bweni shuleni.

"Kwa sasa kuna ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kubeba wanafunzi wa kike 80 na limejengwa kwa nguvu za wananchi na sasa lipo hatua ya lenta, tunaiomba serikali kuangalia namna ya kulikamilisha ili litumike na kuonda adha ya wanafunzi kuangukiwa na nyumba walizopanga mitaani," alisema Mwalimu Lucy.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kahama, ASP Stanley Luhwago alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa alipata taarifa na kufika eneo tukio na kubaini chanzo chake ni ukuta wa nyumba kutokuwa imara na kuangukia ndani ya chumba.

Alisema udhaifu wa ukuta huo ulisababishwa na mvua iliyokuwa inaendelea kunyesha wakati wa usiku, hivyo kusababisha kifo cha mwanafunzi huyo aliyefariki dunia papohapo.

ASP Luhwago aliwataka wakazi wa kata hiyo kujenga nyumba imara za matofali ya kuchoma badala ya udongo ambayo yakilowa yanapukutika, ili kuepukana na majanga ya namna hiyo.

Kufuatia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliagiza Halmashauri kufanya ukaguzi wa nyumba hizo za watu binafsi wanaopangisha wanafunzi na kuhakikisha wanawahamisha waliomo katika nyumba mbovu na zisizo imara.

"Watoto wahamishwe na kupelekwa kwenye nyumba imara na salama kuepukana na majanga ya namna hii kwani nyumba nyingi vijijini zimejengwa kwa udongo, lakini nje zimepigwa plasta na kuonekana ni imara kwa nje, mvua inaponyesha saa 24 zinaanguka," alisema Mhita.

Mkuu wa Wilaya pia aliwataka madiwani kwenye maeneo yao kuwahamasisha wananchi kujenga nyumba za kisasa na kuachana na za udongo.

# Mahakama yaagiza Dk. Slaa kuletwa mahakamani

## -DPP akata rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeagiza kuwa Februari 19 mwaka huu, Dk. Wilbroad Slaa apelekwe mahakamani ili afuatilie kesi yake ya tuhuma kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X.

Dk. Slaa anaendelea kusota rumande katika Gereza la Keko tangu Januari 10 mwaka huu baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuwasilisha mahakamani hati ya kuzuia dhamana yake kwa madai ya "sababu ya usalama wake".

Agizo hilo lilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Rahim Mushi wa mahakama hiyo wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa. Mshtakiwa hakuwapo mahakamani na hali hiyo imekuwa inatokea mara kadhaa.

Kutokana na mshtakiwa kutokuwapo mahakamani kwa mara nyingine, Wakili wa Dk. Slaa, Sanga Melikiole aliomba mahakama mteja wao awe analetwa mahakamani ili afuatilie kesi yake inavyoendelea.

"Ninaagiza Februari 19 mwaka huu mshtakiwa aletwe mahakamani ili afuatilie kesi yake," alisema Hakimu Mushi.

Awali Wakili wa Serikali, Agnes Mtunguja alidai kuwa kesi ililetwa kwa kutajwa na upelelezi haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, Mahakama ya Kisutu imefungwa mikono kuendelea na hatua yoyote kwa sababu DPP amewasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu uliompa unafuu Dk. Slaa katika suala la dhamana.

Inadaiwa kuwa Dk. Slaa alitenda kosa hilo, Januari 9 mwaka huu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mtandao huo wa kijamii, kupitia jukwaa lililosajiliwa kwa jina la Maria Salungi Tsehai @MariaSTsehai kwa lengo la kupotosha umma.

Inadaiwa kuwa kupitia jukwaa hilo, Dk. Slaa alichapisha ujumbe uliosomeka 'wakubwa wametafutana, nikisema wakubwa namaanisha mwamba na Samia, na wala hatuna maneno ya kumung'unya... na kimsingi wamekubaliana, Suluhu Samia amekubali atatoa pesa, Suluhu Samia amekubali ataongeza nguvu ya pesa, ni dhahiri atatoa pesa... hizo ni hela za Watanzania wanazichezea Samia na watu wake.

"Samia toka muda mrefu hahangaikii tena maendeleo ya nchi, anahangaikia namna ya kurudi Ikulu na namna yake ya kurudi Ikulu ni kwa njia hizo kama kumsaidia mtu kama Mbowe".

Inadaiwa kuwa Dk. Slaa, aliyewahi kuwa Mbunge wa Karatu, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na balozi, alisambaza maneno hayo mtandaoni wakati akijua taarifa hizo ni za uongo.



Mmoja wa waliokuwa wateja wa Benki ya FBME, Dk. Majura Mfungo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakiiomba Serikali kutatua mgogoro uliopo baada ya benki hiyo kuungwa na kukosa haki ya pesa zao walizoweka katika benki hiyo. Kulia ni aliyekuwa mteja wa benki hiyo, Deus Okuku na aliyekuwa mfanyakazi wa benki hiyo, Ayubu Nganga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ponda, wenzake waomba kurekebisha kesi kupinga kuwa chini ya BAKWATA

**Na Grace Gurisha**

SHEKHE Ponda Issa Ponda na wenzake 11 wameomba mahakama wafanye marekebisho kwenye hati ya madai kumwondoa Yustadhi Twalib Twalib katika kesi ya kikatiba waliyofungua kupinga kuwa chini Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kutokana na mwenzao huyo kufariki dunia.

Mbali na Sheikh Ponda, wadai wengine Shekhe Ayoub Muinge, Sheikh Prof. Hamza Njozi, Riziki Ngwali, Bakari Shingo, Juma Kilaghai, Abdallah Said, Twalib Twalib, Ibrahim Sherally, Mussa Marua, Abubakar Mngodo na Mustafa Abedib.

Ombi hilo la masheikh hao lilitolewa jana na wakili wao, Juma Nassoro mbele ya Jaji Arnold Kirekiano wa Mahakama Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam wakati shauri hilo lilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa.

"Mheshimiwa Jaji, ninaomba tufanye marekebisho kwenye hati ya madai ili kumwondoa marehemu Twalib Twalib," alidai Wakili Nassoro.

Jaji Kelekiano alikubaliana na ombi hilo na kuwaelekeza kwamba marekebisho hayo wayafanye Februari 12, 2025 na upande wa wadaiwa utajibu Februari 26, 2025 na shauri litasikilizwa Machi 3, 2025.

Wadai hao mbali na Wakili Nassoro, wanawakilishwa pia na Wakili Yahaya Njama, Daimu Hafani, Abdulfattaha A-Bakry na Ubaid Hamidu.

Wamefungua kesi hiyo dhidi ya Msajili wa Vyama vya Kijamii - Wizara ya Mambo ya Ndani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Mkabidhi wa Wasihi Mkuu, BAKWATA na Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania.

Katika hati yao, wanalalamikia kitendo cha mdaiwa wa kwanza, Msajili wa Vyama vya Kijamii na wa pili, Mkabidhi wa Wasihi Mkuu kuwalazimisha waislamu wanaotaka kusajili taasisi yoyote kuwa lazima wapate barua kutoka BAKWATA inayowatambua.

Inadaiwa kuwa katika sheria za Tanzania, hakuna sehemu yoyote inayolazimisha muislamu kuwa chini ya BAKWATA, Baraza hilo limesajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na pia limesajiliwa Rita kama zilivyosajiliwa taasisi zingine. Halina usajili wa kwamba lenyewe ndiyo taasisi ya kuwakilisha waislamu wote Tanzania.

Pia wanadai katika Katiba ya BAKWATA hakuna kipengele chochote kinachoeleza nani ni mwanachama wa BAKWATA na kwamba ukitaka kuwa mwanachama wa BAKWATA, lazima uombe. Hakuna jambo hilo.

"Kwa hiyo kuwalazimisha waislamu kuwa chini ya BAKWATA ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waislamu waachwe wenyewe waamue wanataka kuwa chini ya taasisi gani na wanapotaka kusajili taasisi yoyote ya kidini wasilazimishwe kutambuliwa na BAKWATA.

"Walazimishwe kwa sababu Katiba inatoa uhuru wa mtu yeyote kujiunga na jumuiya yoyote anayoitaka, huwezi kuwalazimisha wawe chini ya BAKWATA, huko ni kuvunja Katiba. Hakuna sheria inayowataka RITA au Msajili wa Vyama vya Kijamii kuelekeza waislamu waende BAKWATA wakalete barua, hakuna sheria hiyo," wanadai katika hati yao.

# HALI INATISHA GOMA

## -Wanawake wabakwa, wachomwa moto
## - 'Mochwari' zajaa, miili yakosa maziko

Na Moshi Lusonzo



Waasi wa M23 wakiwa katika mitaa ya mji wa Goma hivi karibuni. **PICHA: Getty Images**

HALI ya kutisha imeukumba mji wa Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), baada ya maiti za watu kutapakaa katika mitaa mbalimbali baada ya kuuawa na waasi wa M23.

Katika tukio moja, waasi hao walivamia jengo la magereza na kisha kuwabaka wafungwa wanawake 160, wengi wao wamekutwa baada ya waasi kuchoma moto gereza hilo.

Vyumba vya kuhifadhi maiti vimefurika miili ya watu na mingine imerundikana nje kutokana na kuwepo kwa uhaba wa ardhi ya kuwazika.

Inaelezwa karibu watu 3,000 wameripotiwa kuuawa katika makabiliano ya silaha kati ya waasi wa kundi la M23 na wanajeshi wa DRC mashariki mwa nchi hiyo.

Mashirika ya kutoa misaada yalieleza miili ya watu waliouawa inatakiwa kuzikwa haraka iwezekanavyo kutokana na vyumba vya kuhifadhi maiti kufurika.

Katika taarifa yao, walisema hali inahatarisha na kuogofya.

Katika taarifa ya ndani ya Umoja wa Mataifa ambayo BBC ilipata nakala yake, inaonesha kuwa takriban wanawake 165 walishambuliwa wakati wa tukio la kutoroka kwa wafungwa wa kiume.

Idadi kubwa ya wanawake hao walifariki baadaye baada ya jela yao kuchomwa moto, ripoti hiyo ilieleza.

Hata hivyo, hali ya machafuko bado inaendelea katika mji wa Goma na hakuna dalili ya kurudi katika utulivu katika kipindi kifupi kijacho.

**KIVU KUSINI YASHAMBULIWA**

Waasi hao ambao wanaungwa mkono na Rwanda juzi waliuteka mji wenye madini wa Nyabibwe katika jimbo la Kivu Kusini.

Shirika la habari la Reuters liliripoti mapigano hayo yanajiri siku tano baada ya waasi hao kutanganza kusitisha mapigano.

Kutekwa kwa mji wa Nyabibwe unaopakana na Ziwa Kivu kunasababisha waasi kuwa karibu na mji mkuu wa jimbo hilo Bukavu.

Hata hivyo, wiki iliyopita waasi hao walisema kwamba hawana nia ya kuuteka mji huo.

Viongozi wa eneo hilo, wawakilishi wa mashirika ya kiraia, waasi na chanzo kutoka usalama wa taifa, wamethibitisha kuwa Nyabibwe iko mikononi mwa waasi wa M23.

"Kumekuwa na mapigano makali na mji uliangukia mikononi mwa waasi. Wako katikati mwa mji kwa sasa," alisema kiongozi huyo wa mashirika ya kiraia, ambaye kama vyanzo vingine hakutaka kutajwa jina lake.

Nyabibwe, kuna migodi ambayo huzalisha dhahabu, coltan na metali. Pia ni kitovu cha biashara kati ya Goma, mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini na Bukavu.

Waziri wa Mawasiliano wa DRC, Patrick Muyaya aliliambia shirika la habari la Reuters, kuwa waasi walikiuka usitishaji mapigano na wameingia katika mapambano na wanajeshi wa serikali karibu na Nyabibwe.

Corneille Nangaa, kiongozi wa muungano wa waasi wa Congo River Alliance unaojumuisha M23, alithibitisha kuwa kundi hilo limekwenda Nyabibwe.

"Walitushambulia na sisi tukajilinda," aliambia Reuters.

Kwa upande mwingine, mahakama ya kijeshi ya Congo imetoa hati ya kimataifa ya kukamatwa kwa Nangaa ikimtuhumu kwa uhalifu wa kivita na uhaini.

Malawi yaondoa jeshi, Rais wa Malawi Lazarus Chakwera amemuagiza kamanda wa jeshi la nchi hiyo kujiandaa kuondoa majeshi ya Malawi kutoka eneo la Mashariki la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Taarifa hiyo iliyotangazwa katika televisheni ya taifa, ilisema uamuzi wa rais unalenga kuheshimu tangazo la kusitisha mapigano kati ya pande zinazozozana.

Hata hivyo, uamuzi wa kusitisha mapigano uliotangazwa na Waasi wa M23 ulikuwa ni mpango wa kujipanga upya.

Kuondolewa kwa wanajeshi wa Malawi kutatoa nafasi ya mazungumzo yatakayo fanyika kesho ili kupata Amani ya kudumu.

Rais Lazarus Chakwera amekuwa chini ya shinikizo la kuondoa majeshi ya nchi yake Mashariki mwa DRC baada ya wanajeshi watatu wa Malawi kuuawa katika mashambulizi ya M23 mjini Goma.

Wanajeshi hao walikuwa sehemu ya ujumbe wa kulinda amani wa Kusini mwa Afrika uliotumwa na SADC kusaidia serikali ya Congo.

**MAKANISA YAOMBA AMANI**

Wawakilishi wa Makanisa mawili makuu nchini, walisema hakutakuwa na suluhu ya mzozo huo ikiwa wahusika wakuu hawatajumuishwa katika kutafuta suluhu.

Wawakilishi wa Makanisa ya Kikatoliki na Kiprotestanti walitangaza kuanzishwa kwa mashauriano na wadau mbalimbali wa kisiasa, vyama vya upinzani, mashirika ya kiraia na waasi wa M23.

Mchungaji, Eric Nsenga, ambaye ni katibu mkuu wa Kanisa la Kristo nchini Congo (ECC), alisema jukumu la sasa linalotakiwa ni kukaa pamoja na kuzungumza.

"Jukumu letu sio kusema huyu ni malaika, yule ni shetani. Tunataka kupata suluhu, kwa hiyo sielewi kuwa tunazungumzia amani, lakini wakati huo huo tuna mashaka na utaratibu wowote unaoweza kuleta amani. " alisema mchungaji Nsenga.

Alisema katika mtazamo wao, wanalenga amani ya kudumu. Vyovyote iwavyo, itakuwa ni jambo la uwongo, kufikiria kuwa na amani bila kujumuisha wadau wote wanaohusika.

**ICC YAFUATILIA KARIBU**

Ofisi ya mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) imesema inafuatilia kwa karibu hali inayoendelea nchini DRC, ikieleza kuwa vyanzo vya kuaminika vinaonesha kuwa mamia ya watu wameuawa katika ghasia zinazoendelea.

"Ofisi inafuatilia matukio ya sasa kwa karibu, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa ghasia katika wiki za hivi karibuni mashariki mwa DRC, hasa ndani na karibu na Goma," ilisema katika taarifa yake.

Mwendesha Mashtaka wa ICC, Karim Khan, alitangaza kwamba Ofisi hiyo itarudia juhudi zake za uchunguzi nchini DRC, kwa kuzingatia madai ya uhalifu chini ya Mkataba wa Roma yaliyoripotiwa katika mkoa wa Kivu Kaskazini tangu Januari 1, 2022.

"Uchunguzi huu unaolengwa umeanzishwa na unaendelea kwa dharura," kilisema chanzo kimoja.

Vyanzo vya kuaminika vinaonesha kuwa maelfu ya watu wamejeruhiwa na mamia wameuawa ndani na karibu na Goma, wakiwemo raia na walinda amani katika mapigano hayo.

# Mbunge aibana serikali mazao kuoza shambani

Na Jenifer Gilla

MBUNGE wa Viti Maalum, Sofia Mwakagenda, ameitaka serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa mazao yanayoharibika haraka kama vile parachichi na chai yananunuliwa kwa wakati shambani ili kuepusha hasara kwa wakulima.

Sophia alitoa hoja hiyo jana bungeni kupitia swali alilomuuliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akihoji serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa mazao yananunuliwa kwa wakati shambani ili kuepusha yasioze.

Alisema baadhi ya mazao yamekuwa yakipata bei nzuri na kuwapatia wakulima faida wanayoitaka ila kumekuwa na wanunuzi ambao wamekuwa wakichelewa kuyanunua na kusababisha kuoza na kuwatia hasara.

Kutokana na hali hiyo, Mbunge huyo aliishauri serikali kutoa kauli ili kuwabana wanunuzi ambao wanachelewa kuyanunua kwa makusudi ili yashuke bei na matokeo yake mazao yanaozea shambani.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu, alisema mkakati wa serikali kupitia Mamlaka ya Mazao ya Bustani (TAHA) inahamasisha uwekezaji wa viwandani ili kuhakikisha yananunuliwa kwa wakati mashambani na kuchakatwa ili yasiharibike.

"Kwa hiyo utaratibu ambao tunauweka sasa ni kuhamasisha uwekezaji kwa mazao ya kilimo kama vile maparachichi," alisema.

Alisema mpaka sasa kuna viwanda vya uchakaji wa mazao Njombe na Mufindi na wanatarajia kujenga kingine Kilolo na uwapo wake umechangia mazao hayo kutoharibikia shambani.



Wataalamu na wahadhiri wa vyuo vikuu mbalimbali nchini, wakipitia mtaala wa Shahada ya Uzamivu (PhD) ya Infomatiki za Biashara, ulioandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kutoa maoni yao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CBE kuanzisha shahada ya uzamivu ya biashara

Na Joseph Mwendapole

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kinatarajia kuanzisha shahada ya uzamivu (PhD) katika infomatiki ya biashara ili kuleta mabadiliko ya uchumi wa kidijitali na teknolojia katika kufanya biashara kulingana na mabadiliko ya dunia.

Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo ya kujadili mtaala wa masomo hayo yaliyowashirikisha wataalamu wabobezi kutoka taasisi mbalimbali za elimu ya juu.

Wataalamu hao walikuwa wakipitia mtaala ambao umeandaliwa na chuo hicho na kutoa maoni yao ili baada ya hapo upelekwe kwa mdhibiti ambaye ni Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTIVET) kwaajili ya kupewa ithibati na kuanza kutumika.

Alisema kuanzishwa kwa shahada hiyo ni hatua muhimu yenye kuleta mabadiliko katika kuendeleza elimu ya juu, kukuza uvumbuzi wa kiteknolojia na kuchangia ajenda ya maendeleo ya taifa.

Prof. Lwoga alisema CBE ambayo ina kampasi nne nchini kwa muda mrefu imekuwa kinara katika kutoa program mbalimbali za kitaaluma na kwa kushirikana na Chuo Kikuu cha Ufini ya Mashariki kimeandaa mtaala wa informatiki za biashara.

Alisema shahada hiyo ya infomatiki za baishara ni muhimu kwa kuwa inachanganya utaalamu wa biashara na uvumbuzi wa kiteknolojia ikilenga uchanganuzi wa data, mifumo ya habari, mabadiliko ya dijiti na utafiti unaotegemea suluhisho.

"Wahitimu wa program hii wanatafutwa sana kwenye sekta ya umma na binafsi na watakuwa wahusika wakuu katika kuleta mabadiliko ya teknolojia katika tasnia mbalimbali nchini," alisema.

Alisema mtaala huo utawapa wanafunzi wa Tanzania ujuzi unaohitajika ili kuendesha na kuongoza katika uchumi wa kidijitali na kuchangia katika uboreshaji wa maendeleo ya viwanda.

Mtaala huo, utasaidia kuongeza tija katika biashara za kidijitali na kuimarisha ushindani wa kimataifa pamoja na kuongeza ujuzi katika kufanya tafiti na uvumbuzi wa kiteknolojia katika sekta ya biashara za kidijitali.

"Mkutano huu ni muhimu katika kuunda mustakabali wa program hii na maoni yenu wadau yatasaidia kuunda mtaala unaoakisi mahitaji ya soko la ajira na kuendana na malengo ya maendeleo Tanzania," alisema.

Alisema wanatarajia baada ya kupata ithibati mtaala huo utaanza kutumika hapa nchini na utakuwa mtaala wa kwanza kwenye biashara ya infomatiki ambao utaenda kuzalisha wataalamu watakaokuwa watafiti wabobezi katika uvumbuzi wa kiteknolojia na kuangalia mifumo itakayosaidia kwenye biashara.

"Hivi sasa teknolojia inabadilika kwa haraka sana na kuna akili mnemba (AI) yote tumeyazingatia kwenye huo mtaala na juhudi kama hizi tulianza mwaka 2014 ambapo tuliingia makubaliano na chuo cha Finland Mashariki ambao wanatoa program hii muda mrefu.

"Walitusaidia sana kuwapa mafunzo wataalamu wetu ambao tumekuwa tukiwapeleka kwenye chuo hicho na mpaka sasa tuna walimu wengi ambao wameshahitimu kwenye shahada ya infomatiki ya biashara Finland na sita bado wanaendelea na masomo yao huko huko," alisema.

Dk. Angela Runyoro, Mhadhiri Mwandalizi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), alisema mitaala hiyo itawezesha kuwafundisha watu kutoka ndani na nje ya nchi kupata ujuzi wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA katika biashara.

"Kwa sasa TEHAMA inahitajika katika sekta zote, hakuna namna unaweza kufanya jambo ukaikwepa na CBE wenyewe wamejikita kuanza kutengeneza wataalamu wa infomatiki za biashara kwa kujua mifumo ya kuendesha biashara kisasa,"alisema

"Hawa wataalamu watafundisha wengine watafanya tafiti watachambua mifumo inayofaa katika teknolojia ya kustawisha biashara ili watu wasifanye baishara kizamani . Hii itakuwa na manufaa sana kwa wafanyabiashara na nchi na ulimwengu kwa ujumla," alisema Runyoro.

# TFRA yatakiwa kutatua vikwazo upatikanaji mbolea ya ruzuku

Na Mwandishi Wetu, MOROGORO

MWENYEKITI wa Bodi Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) amewataka watendaji wa mamlaka hiyo kutatua changamoto za wakulima katika upatikanaji mbolea ya ruzuku ili kutimiza malengo ya serikali kuinua sekta ya kilimo nchini.

Anthony Diallo wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi cha Mamlaka hiyo kilichofanyika mjini hapa juzi.

Diallo alisema vikao hivyo ni fursa muhimu kwa watumishi hao kutathmini mafanikio ya mamlaka hiyo na kupanga mikakati ya kuboresha utendaji kazi wa mwaka na kufanikisha malengo yao.

Alisema TFRA inapaswa kuweka vipaumbele vya kibajeti katika masuala ya kimkakati na kumsaidia mkulima kupiga hatua katika kilimo kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea.

"Ni muhimu kuhakikisha tunatatua changamoto za wakulima kabla hazijawa mzigo kwao, tupo kwa ajili ya kuwahudumia kwenye mnyororo wa pembejeo ya mbolea," alisema.

Aliwataka kuweka mikakati ya kuwa na vifaa vya kuhakiki taarifa za wakulima kuhusiana na mahitaji ya mbolea katika maeneo wanayosimamia, kuimarisha huduma na kuleta tija katika sekta hiyo ya mbolea nchini.

Diallo aliwataka wajumbe wa baraza hilo kufanya tathmini ya utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa kwenye kikao kilichopita na kuhakikisha maamuzi yanayofikiwa yanatekelezwa kikamilifu kwa manufaa ya sekta ya kilimo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alitaja lengo kuu la kikao hicho kuwa ni kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 na mapendekezo ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026 na kuwasilishwa kwenye bodi kufanyiwa mapitio na kuidhinishwa.

Laurent alisema kikao cha mwaka huu kilitanguliwa na mafunzo kwa wajumbe wa baraza hilo ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kama wawakilishi wa vitengo na idara ndani ya mamlaka hiyo.

Alisema kikao hicho ni jukwaa muhimu kwa kuwa kinapokea maoni yanayoakisi hali halisi ya utendaji wa taasisi na kujumuisha ushiriki wa ngazi zote za watendaji.

"Hii ni fursa ya kujadili jinsi ya kuimarisha utendaji wetu ili kuhakikisha huduma kwa wakulima zinaendelea kuwa bora zaidi," alisema Laurent.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ichukuliwe ulaji wa nyama nguruwe kuepuka kifafa

**FEBRUARI** 10 kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya Kifafa Duniani ambayo huadhimishwa kwa lengo la kutoa takwimu kuhusu madhara ya ugonjwa huo na hatua gani zinapaswa kuchukuliwa katika kupambana na tatizo hilo.

Ugonjwa wa kifafa husababishwa na mambo mbalimbali yakiwamo ulaji nyama ya nguruwe isiyoiva ipasavyo, ajali, uzazi pingamizi na mbung'o katika baadhi ya maeneo hasa ya kitropiki ambayo huchangia kuzaliana kwa wadudu hao.

Takwimu zinaonesha kuwa kifafa ni ugonjwa wa kudumu wa ubongo unaoathiri takribani watu milioni 60 na inakadiriwa kwamba watu 34 hadi 76 kwa kila wagonjwa 100,000 wapya wanaongezeka kila mwaka, ukiwa ni wastani wa uwiano wa asilimia 0.5 hadi moja.

Nchini Tanzania, athari ya jumla ya muda wote ni asilimia mbili huku Afrika ikiwa na idadi kubwa ya walioathirika ambao ni kati ya watu 20 na 58 kwa kila watu 1,000. Utafiti uliopita na wa sasa umeonesha kuwa takribani watu milioni moja wanaishi na kifafa nchini.

Aidha Mahenge katika wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro na Hydom, Mbulu mkoani Manyara yanatajwa kuwa ni maeneo yanayoongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa. Ulanga ina wagonjwa wengi kutokana na ongezeko la mazalia ya mbung'o huku Hydom ikitajwa kuwa inaongoza kwa ulaji wa nyama ya nguruwe, ikiwamo ile isiyoiva kwa kiwango kinachotakiwa.

Taarifa zinabanisha kwamba kitimoto (nyama ya nguruwe) isipoiva ipasavyo, husababisha minyoo ambayo husafiri hadi kichwani na kuziba damu kupita ipasavyo. Kutokana na hali hiyo, mlaji wa nyama hiyo, hasa ambayo haijaandaliwa kwa ufasaha na kuiva kwa kiwango kinachotakiwa, mlaji anaweza kukumbwa na ugonjwa huo.

Takriban miaka 30 sasa, nyama ya nguruwe, maarufu kama kitimoto,imejipatia umaarufu mkubwa nchini na kupendwa na watu wengi. Watu wengi wamekuwa wakifika kwenye sehemu za starehe kama vile baa ambako nyama hiyo imekuwa ikiuzwa kwa wingi kama asusa au mlo kamili sambamba na ugali au ndizi.

Pia zimeanzishwa bucha mbalimbali za nyama hiyo kila kona hasa kwenye miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Morogoro na Iringa. Jambo la kujiuliza ni je, kuwapo kwa biashara hiyo katika maeneo mbalimbali, wahusika wana uelewa kuhakikisha nyama hiyo inaiva ipasavyo na kutoathiri watu kukumbwa na maradhi mbalimbali, ikiwamo kifafa?

Kwa ujumla, biashara ya nyama ya nguruwe, kitimoto kama inavyojulikana, inashika chati ya juu katika ulaji kwa sasa lakini kutokana na taarifa kwamba ni moja ya vyanzo vya maradhi ya kifafa, tahadhari inapaswa kuchukuliwa ili isisababishe madhara kwa binadamu hasa watumiaji.


Kama Chama cha Wataalamu wa Kifafa Tanzania (TEA) kilivyoainisha tatizo hilo, ni vyema elimu ikatolewa kuanzia muuzaji wa nyama hadi mtumiaji ili kuhakikisha uandaaji wa kitoweo hicho unafanyika katika viwango vinavyotakiwa ili kutoleta madhara ya kiafya.

Kutokana na nyama hiyo kupendwa na watu wengi, hivyo imechangia kuwapo kwa ajira kuanzia wafugaji, wachinjaji na wauzaji. Kwa mantiki hiyo, suala hapa si kukataza watu kutumia bali kuhimiza iandaliwe kwa viwango stahiki ili isisababishe maradhi yakiwamo ya kifafa.

Suala la afya bora linaanza na mtu mmoja mmoja kisha jamii na taifa kwa ujumla ikiwamo kuchukua tahadhari kuhusu matokeo ya jambo fulani. Kwa hiyo katika kujikinga na kifafa kupitia ulaji wa nyama ya nguruwe ambayo haijaiva kama inavyotakiwa, ni vyema kila mtu achukue hatua kujilinda na tatizo hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# La Vijana 600 kunolewa kwa 'Jenga Tanzania Bora', idadi ifike maelfu!

**SERIKALI** imepanga kuwatumia vijana waliopata mafunzo na kurasimisha ujuzi katika kada mbalimbali kusaidia katika ukarabati wa miradi mbalimbali nchini.

Patrobas Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, alisema hayo wakati akijibu maswali bungeni, jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa vijana zaidi ya 600 wamepatiwa ujuzi katika mradi ya 'Jenga Kesho iliyo Bora (BBT)'.

Alisema kada ambazo zimepatiwa mafunzo, ni pamoja na fundi seremala, ufundi uashi, ujenzi na zaidi ya vijana 500, wamepatiwa vyeti baada ya kuhitimu.

Akasema huo ni mpango wa kuboresha mazingira ya kisera kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo na kuweza kujitegemea, kupitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na Sera ya Taifa ya Ajira.

Niipongeze serikali kwa mpango huo, pamoja na mheshimiwa Katambi kwa kujibu swali hilo kwa ufasaha na kueleweka kirahisi mno.

Ushauri wangu ni kwamba, serikali iangalie zaidi kuwasaka vijana wenye vipaji zaidi kwa ajili ya mafunzo hayo.

Nikisema wenye vipaji, nina maana halisi ya kiti hicho. Wapo vijana wanaweza kupata mafunzo awali wakiwa hawajui lolote kuhusu wanachokwenda kujifunza, lakini baada ya mafunzo wakawa mafundi wazuri tu.

Lakini wapo ambao wana vipaji wa jambo husika kabla ya kwenda kujifunza.

Iwapo mradi ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT), itaweza kuwapata vijana wa aina zote mbili, wa kawaida na wale wenye vipaji husika, basi kuna manufaa makubwa ambayo taifa letu litapata baadaye.

Katika dunia hii, Mungu amewaumba binadamu kila mmoja na kipaji chake, lakini kwa sasa inaonekana wenzetu nje ya nchi hasa huko tunakoendelea, wamekuwa wakitumia zaidi vipaji vya wananchi wao kuziendelea nchi zao.

Maendeleo ya sayansi ya teknolojia tunayoyaona sasa yanatokana na kuwa na watu ambao wamewachukua bado wadogo baada ya kuona vipaji vyao, hivyo kuwaendeleza kimafunzo.

Yeyote mwenye kipaji fulani, akiendelezwa, anakuwa si tu anafahamu alichojifunza, lakini pia anakuwa mbunifu, na hata akifanya akipata kazi, anaifanya kwa moyo, kujitolea na kujituma kwa sababu anafanya kitu ambacho anakipenda.

Wanafanya kazi hizo mara nyingi hawajali sana maslahi yao binafsi, bali kusaidia watu, pamoja na manufaa ya nchi.

Anayefanya kazi ambayo msingi wake ni kipaji, mara nyingi hachoki, kwani hatumii nguvu nyingi kufanya na kufikiri, hivyo taifa na wananchi wake wananufaika na uwezo wake.

Tunaona wenzetu ambao wanatengeneza ndege, magari, vyombo vikubwa vya usafiri, vifaa vya ulinzi na usalama, msingi wote huo ni kupatikana kwa watu sahihi wenye vipaji, ambao wanachukuliwa na kuanza kupatiwa mafunzo sahihi na kwa wakati sahihi.

Kwa maana hiyo, naishauri BBT, ijielekeze humo, na niwaibie siri tu mara nyingi vipaji huwa kwa watu ambao wametoka kwenye mazingira au familia za kimasikini.

Mfano mdogo tu, angalia hata kwenye soka, au muziki, huwezi kukuta, mtoto anayetoka familia ya kitajiri anakuwa mwanamuziki, au mchezaji soka. Na kama wapo ni wachache mno, na hawawezi kuwa wanamuziki au wachezaji mahiri.

Hii ndiyo hata kwenye nyanja zingine. BBT, iende ndani zaidi isake pia vijana wa kimasikini wenye vipaji mbalimbali, kama ushonaji, ufundi, na vitu vingine vinavyofanana na hivyo ili hata kama ikipata wahitimu.

Basi wawe na wahitimu siyo wenye uwezo wa kushona, ufundi seremala, au fundi makenika tu, bali kupata wabunifu ambao wanaweza kufanya kitu ambacho nchi ikatikisika na kunufaika naye. Hawa watoto au vijana wapo, ila tu hawafikiwi kirahisi. Kama jitihada zitafanyika kuwasaka watapatikana na baada ya miaka kadhaa, nchi itajivunia nao kupitia mradi huo wa BBT.

TANGAZO

MuCoBa Bank PLC

*"Kwa Maendeleo Yako"*

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/12/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31/12/2023 | Mwaka Uliopita 31/12/2022 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 433 | 239 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 107 | 13 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,733 | 2,393 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 14,818 | 15,641 |
| 12 | Mali nyingine | 3,616 | 3,738 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 374 | 514 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **21,081** | **22,538** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 13,304 | 14,060 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 86 | 86 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 110 | 186 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 537 | 503 |
| 28 | Madeni | 3,515 | 3,776 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **17,555** | **18,614** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,526** | **3,924** |
| | | | |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | | |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,589) | (5,724) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (395) | 181 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 721 | 677 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | **3,526** | **3,924** |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | | |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,526 | 1,544 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 191 | 171 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | | |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 16.73% | 17.41% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 10.30% | 9.87% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 32.64% | 111.24% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 17.15% | 69.40% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 87.95% | 84.61% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -5.38% | -13.78% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -6.46% | -7.21% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/12/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31/12/2023 | Mwaka Uliopita 31/12/2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,253 | 3,014 |
| 2 | Gharama za Riba | (553) | (734) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 1,700 | 2,280 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (192) | (190) |
| | | | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 868 | 890 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 868 | 890 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(2,771)** | (2,793) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,275) | (1,243) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (72) | (54) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,424) | (1,496) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | (395) | 187 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | (6) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | (395) | 181 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | (395) | 181 |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 50 | 56 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | - | 6 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | -88.96% | 36.38% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | -10.60% | 4.61% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 94.94% | 76.41% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | -16.06% | 6.84% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/12/2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31/12/2023 | Mwaka Uliopita 31/12/2022 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | (395) | 187 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | Hasara Katika Mali | 920 | 409 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 631 | (780) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (759) | (2,260) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (53) | (334) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 118 | 351 |
| | Kodi Iliyolipwa | (113) | (120) |
| | Mengineyo (Bainisha) | (387) | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **(38)** | **(2,547)** |
| | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 25 | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (48) | (195) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | 25 | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(23)** | **(195)** |
| | | | **-** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | **-** |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **(2,111)** | (200) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | **1,800** | 1,450 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | **-** | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | **-** | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | **-** | - |
| | Mengineyo (bainisha) | **-** | (4) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(311)** | **1,246** |
| | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (372) | (1,496) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Mwaka | 2,645 | 4,141 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Mwaka | **2,273** | **2,645** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31/12/2023
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,791** | **(5,543)** | **675** | **3,924** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (395) | - | **(395)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | (45) | 45 | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | (2) | - | **(2)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,791** | **(5,986)** | **720** | **3,526** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2022** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,795 | (4,558) | 108 | **4,344** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 181 | - | **181** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | (4) | - | - | **(4)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | (568) | 568 | **-** |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | (598) | - | **(598)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,791** | **(5,543)** | **675** | **3,924** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/12/2023

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Denis Rweyendera ........................................ Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | **18/Jan/2025** |
| Kelvin Mushi ........................................ .... Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | **18/Jan/2025** |
| Saleh S Abdallah................................................ Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | **18/Jan/2025** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Bakar R. Bakar.......................................................... (Imesainiwa) Mkurugenzi | **18/Jan/2025** |
| 2. Prof. Dominicus Kasilo........................................ (Imesainiwa) Mkurugenzi | **18/Jan/2025** |

MuCoBa Bank PLC
"Kwa Maendeleo Yako"

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-03-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa<br>31/03/2024 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita<br>31/12/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 386 | 239 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 9 | 13 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,452 | 2,393 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 14,221 | 15,641 |
| 12 | Mali nyingine | | 3,738 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 3,670 | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | | - |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 304 | 514 |
| | | **20,041** | **22,538** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 12,564 | 14,060 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | - |
| 20 | Amana Maalumu | 49 | 86 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 143 | 186 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 340 | 503 |
| 28 | Madeni | 3,368 | 3,776 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **16,467** | **18,614** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,573** | **3,924** |
| | | | |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | | |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,984) | (5,724) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 47 | 181 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 721 | 677 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | | |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **3,573** | **3,924** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 971 | 930 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 167 | 172 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 17.83% | 16.96% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 10.46% | 10.30% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 118.49% | 115.92% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70.96% | 70.36% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 90.15% | 90.60% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -6.15% | -16.18% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -4.93% | -8.43% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-03-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa<br>31/03/2024 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita)<br>31/03/2023 | Limbikizo lamwaka sasa<br>31/03/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita)<br>31/03/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 520 | 490 | 520 | 490 |
| 2 | Gharama za Riba | (94) | (178) | (94) | (178) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **426** | **312** | 426 | 312 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | | (197) | - | (197) |
| | | | | | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **212** | **198** | 212 | 198 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 212 | 198 | 212 | 198 |
| | 6.3 Gawio | | - | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | | - | | |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(590)** | **(726)** | (590) | (726) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (272) | (392) | (272) | (392) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | | (25) | - | (25) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (318) | (309) | (318) | (309) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **47** | **(413)** | 47 | (413) |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | (10) | - | (10) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **47** | **(423)** | 47 | (423) |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **47** | **(423)** | 47 | (423) |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | | 55 | - | 55 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | - | - | - | - |
| 15 | Idadi ya Matawi | - | - | - | - |
| | | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | | | | |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 0.23% | -2.01% | 0.23% | -2.01% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 1.33% | -23.13% | 1.33% | -23.13% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 80.66% | 105.50% | 80.66% | 105.50% |
| | | 2.57% | 1.88% | 2.57% | 1.88% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-03-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa<br>31/03/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita<br>31/12/2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa<br>31/03/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita)<br>31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 47 | 135 | 47 | 135 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | - | |
| | Hasara Katika Mali | 71 | 51 | 71 | 51 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 598 | (88) | 598 | (88) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (823) | (2,584) | (823) | (2,584) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (119) | 82 | (119) | 82 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (55) | 80 | (55) | 80 |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | (280) | (2,324) | **(280)** | **(2,324)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (51) | - | (51) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **(51)** | **-** | **(51)** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (145) | (375) | (145) | (375) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | 850 | - | 850 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | (145) | **475** | **(145)** | **475** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | **(425)** | **(1,900)** | **(425)** | **(1,900)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwa | 2,272 | 4,171 | 2,272 | 4,171 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwa | **1,847** | **2,272** | **1,847** | **2,272** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-03-2024
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **46** | - | **46** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,937)** | **721** | **3,573** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,789 | (5,543) | 676 | 3,922 |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (395) | - | (395) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | (45) | 45 | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| **Jina Na Cheo** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Denis Rweyendera<br>Meneja Mkuu | .................................. (Imesainiwa) | **18/Jan/2024** |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | ..................................... (Imesainiwa) | **18/Jan/2024** |
| Saleh S. Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ................................. (Imesainiwa) | **18/Jan/2024** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| **Jina** | **Tarehe** |
|---|---|
| 1. Bakar R Bakar.....................(Imesainiwa)<br>**Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi** | :<br>6/Feb/2024 |
| 2.Prof. Dominicus Kasilo ........................(Imesainiwa)<br>**Mkurugenzi** | **6/Feb/2024** |



# Jela maisha kwa kubaka watoto watatu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara imemhukumu mkazi wa Bonga, Steven Samweli (21), kutumikia kifungo cha maisha gerezani baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kuwabaka watoto watatu (majina yamehifadhiwa).

Mshtakiwa huyo anadaiwa kuwabaka watoto wawili wenye umri wa miaka tisa na mwingine mwenye miaka 10.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema mshtakiwa ametiwa hatiani na mahakama baada ya kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka na upande wa utetezi.

Kimario alisema katika kosa la kwanza mpaka la tatu, mshtakiwa ametiwa hatiani kwa kosa la kubaka watoto watatu, ambao aliwabaka kati ya Julai hadi Agosti mwaka jana kwa nyakati tofauti katika nyumba moja.

Alisema kwa kipindi hicho mshtakiwa alifanya kitendo hicho na watoto watatu wa shule na alipoulizwa mahakamani alikana mashtaka yanayomkabili.

Aidha, alisema mahakama ilijiridhisha baada ya kusikiliza mashahidi wanane wa upande wa mashtaka na mashahidi watatu upande wa utetezi.

"Mahakama imemtia hatiani mshtakiwa baada ya kusikiliza mashahidi wote akiwemo daktari ambaye alithibitishia mahakama kuwa watoto hao waliingiliwa, japo michubuko ilikuwa ya muda mrefu," alisema Kimario.

**"Mahakama imemtia hatiani mshtakiwa baada ya kusikiliza mashahidi wote akiwemo daktari ambaye alithibitishia mahakama kuwa watoto hao waliingiliwa...**

Hakimu huyo alisema watoto hao waliiambia mahakama kuwa walichukuliwa kutoka njia panda ya Ayasanda na mshtakiwa alipokamatwa alikutwa nyumba ile walipokutwa watoto.

"Kila kosa moja na kutia hatiani na kutumikia kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kwanza na la pili, na kwa kosa la tatu na kutia hatiani kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani," alisema Kimario.

Wakili wa serikali, Blandina Msawa, alisema hawana kumbukumbu ya makosa ya nyuma ila aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu inayotajwa na sheria na mahakama kuwa afungwe kifungo cha maisha.

Wakili Msawa alidai kuwa mshtakiwa alikiuka Kifungu cha 130 (1), (2) (e) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo Mwaka 2022.

Wakili wa utetezi, Erick Machiwa, aliiomba mahakama katika hukumu atakayoitoa mahakama izingatie mshtakiwa ni kijana mdogo, na ni kosa la mara ya kwanza na nguvu kazi ya taifa bado inaweza kusukuma gurudumu.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga, Ramadhani Ndwatah (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga jana, wakati akitoa taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo, kwa kipindi cha miezi miwili kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba mwaka 2024. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Serikali yaonya watakao wanyanyasa wanawake

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha imesema itachukua hatua kali dhidi ya watu au maofisa wa umma watakaofanya unyanyasaji dhidi ya wanawake watakaojitokeza kutoa huduma mbalimbali, kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Kitaifa yatakayofanyika mkoani hapa Machi 8 mwaka huu.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Misaile Musa alitoa onyo hilo wakati wa kikao maalumu cha maandalizi ya maadhimisho hayo ambayo Rais Samia Hassan Suluhu, anatarajia kuwa mgeni rasmi.

"Tunaunda kamati ya kuratibu maadhimisho haya, lakini nawaomba wanawake mjitokeze kwa wingi katika makongamano na maonyesho haya kubwa zaidi.

Wanawake mpendane na msisite kutoa taarifa yoyote ile, iwe ya unyanyasaji au ukosefu wa huduma kutoka kwa maofisa wetu, ili sisi viongozi tuchukue hatua kumaliza tatizo," alisema.

Februari 3 mwaka huu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema maadhimisho hayo kwa mwaka huu, yatakuwa ya namna ya kipekee yakibeba sura tofauti kwa kuwa yanaambatana na miaka 30 ya utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing (1995). Maadhimisho hayo yanatanguliwa na kaulimbiu isemayo, 'wanawake na wasichana tuimarishe usawa, haki na uwezeshaji.'

Waziri Gwajima, alisema lengo la kaulimbiu hiyo, ni kuhamasisha jamii kukuza usawa, haki na uwezeshaji wa wanawake na wasichana; na kwa kuzingatia kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2025 ili, wajiamini, wajiandae na wajitokeze kugombea nafasi za uongozi.

Alisema Machi 3 hadi 6, yatafanyika makongamano ya kikanda katika kanda saba; na mikoa itakayohusika ni Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Geita, Mbeya, Lindi na Kigoma; na kila mkoa utakuwa na ajenda zao, ambazo zitatangazwa kwa ajili ya kujadiliwa kwenye makongamano hayo.

Kadhalika alisema Machi 5 hadi 8, kutakuwa na maonyesho ya wanawake, taasisi za umma na binafsi na kampuni mbalimbali yatakayofanyika mkoani Arusha na Machi saba kumeandaliwa usiku maalum wa mwanamke ambao unatarajiwa kuhudhuriwa na watu takribani 1,500 mkoani Arusha.

# Vijana 50 wajengewa uwezo ufundi wa umeme

**Na Hamida Kamchalla**, MKINGA

HATIMAYE Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, imeanza kupata ahueni katika utatuzi wa changamoto ya uhaba wa mafundi wa huduma ya kuunganisha umeme majumbani, baada ya kujengewa uwezo vijana 50 kupitia Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Nchini (VETA).

Mkuu wa wilaya hiyo, Gilbert Kalima, alisema vijana hao kwa sasa wanapita vijijini kutoa huduma hiyo na wamekuwa wakisaidia kuwaunganishia wananchi umeme bila tozo, kama njia ya kurudisha fadhila kwa wananchi.

Kalima alikuwa akizungumza jana katika maadhimisho ya miaka 30 ya VETA katika viwanja vya chuo hicho. Aliwakilishwa na Ofisa Tarafa ya Mkinga, Heugen Mkinga.

"Ndugu zangu, kwa Mkinga vijiji 85 vimeshasambaziwa umeme, bado vitongoji. Ni imani yangu, wale vijana 50 wanaosomeshwa hapa kutawasaidia wananchi na kutatua kero walizokuwa wanazipata.

"Awali kabla chuo hiki hakijajengwa hapa; tulikuwa tunafuata mafundi umeme kutoka Wilaya ya Tanga, lakini tuna imani wananchi watakwenda kuipata huduma ile kwa karibu na kwa wakati." alisema


Mbali na vijana hao, Kalima, alisema VETA Wilaya ya Mkinga, mbali na mafunzo mbalimbali yanayotolewa, kimekuwa kikiimarisha shughuli zinazofanywa na wananchi wa wilaya hiyo kwa kuongeza thamani madini ya mawe. Alisema ipo haja ya kuupongeza uongozi wa chuo hicho, kwani kimekuwa kikiongeza kipato kwa wananchi kupitia madini hayo yanayojulikana kama tanga stone.

"Kwa kuongeza thamani tunakwenda kuongeza kipato na kuwainua wananchi wa Mkinga ambao wanatapa tabu nyingi sana kuyatafuta mpaka kuyapata hayo mawe," alisema Kalima.

Kalima, alibainisha kwamba yapo mambo ya kujivunia ambayo yanaonekana kupitia chuo hicho kwa kuzalisha vijana ambao tayari wameshakuwa msaada mkubwa kwa jamii zinazowaangukia.

Naye, Mkuu wa Chuo hicho, Kalvin Haule, alisema chuo kina uwezo wa kudahili wanafunzi 240 wa mafunzo ya muda mrefu, ambapo 144, wanaishi katika mabweni ya chuo.

Alisema: "Lakini pia tunatoa mafunzo ya muda mfupi ambapo chuo kinadahili wanafunzi wapatao 100 kwa mwaka kwa kuzingatia mahitaji ya shughuli za kiuchumi kwa Wilaya ya Mkinga".





# TAKUKURU yaibua ufisadi uuzaji viwanja Kahama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga imeokoa kiasi cha Sh. milioni 137.8 kutoka kwenye mauzo yasiyo sahihi ya viwanja katika Manispaa ya Kahama.

Hayo yalibainishwa juzi na Kamanda wa TAKUKURU wa Mkoa huo, Donasian Kessy wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ya kipindi cha robo ya pili kuanzia Oktoba hadi Desemba 2024/2025.

Donasian, alisema kwa kipindi hicho, wamefanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha ikiwa ni sehemu ya fedha za mauzo ya viwanja 29 vilivyopimwa na Manispaa hiyo mwaka 2019.

Alisema katika viwanja hivyo ilitolewa gharama halisi ambayo wananchi wangepaswa kulipa, lakini viwanja vitatu ndiyo vililipwa fedha halisi, huku 26 malipo yakiwa siyo sahihi.

"Manispaa ya Kahama ilikuwa ikimiliki ardhi katika eneo la kimkakati la Phantom, na mwaka 2019 iliamua kupima na kuuza viwanja 29 kwa wananchi kwa gharama ya Sh. 15,000 kwa mita moja ya mraba, na viwanja vya biashara Sh.20,000," alisema na kuongeza kuwa:

**"Manispaa ya Kahama ilikuwa ikimiliki ardhi katika eneo la kimkakati la Phantom, na mwaka 2019 iliamua kupima na kuuza viwanja 29 kwa wananchi kwa gharama ya Sh. 15,000 kwa mita moja ya mraba, na viwanja vya biashara Sh.20,000,"**

"Mwaka 2024 TAKUKURU kupitia vyanzo vyetu vya siri, tulipata taarifa baadhi ya wananchi wamemilikishwa viwanja hivyo bila ya kulipa gharama halisi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Manispaa ya Kahama,tulibaini kuwa viwanja vitatu pekee wamiliki wake walilipa malipo halali, lakini 26 havikulipwa gharama halisi vyenye thamani ya Sh. milioni 800." Alisema baada ya kubaini hilo, waliwafikia wamiliki wa viwanja hivyo na kuwataka walipe gharama halisi ya mauzo ya viwanja hivyo au vitangazwe upya. Alisema wamiliki hao walikubali kufanya malipo halisi Sh.milioni 137.8 kati ya Sh.milioni 800.

Alisema TAKUKURU inaendelea kufuatilia fedha zilizobaki Sh. milioni 662.2 ili kuhakikisha viwanja vyote vinalipiwa na kuingizwa serikalini.

Akizungumzia upande wa dawati la uchunguzi, alisema walipokea malalamiko 38, kati ya hayo ya rushwa 20 na mengine 18 na kwamba uchunguzi wake unaendelea. Alisema wamejipanga kuzuia rushwa kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini mwaka huu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Mohamed Mchengerwa (katikati), akiwa kwenye darasa la awali la shule ya Bahi ya mchepuo wa kiingereza, wilayani Bahi, mkoani Dodoma jana, baada ya kuzindua madarasa ya awali 18 yaliyojengwa na Serikali ya Uingereza kupitia Mradi wa Shule Bora kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni 300. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wakulima wapata faida kuuza choroko kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

WAKULIMA wa Choroko wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu kwa mara ya kwanza wameuza zao hilo na kusifu kuwa kuna faida tofauti na kawaida.

Hayo yalibainishwa na Mkulima Mwitagula Mwitagula wakati wa mnada huo uliofanyika katika ghala la Dutwa lililopo wilayani humo.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, aliishukuru serikali kwa kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), minada hiyo na kuleta faida kwa mkulima na mnunuzi.

"Mfumo huu ni mzuri sana kwa sababu ni wa wazi, mkulima anauza mazao yake bila wasiwasi wowote na kuwa na uhakika na biashara anayofanya,"alisema Mwitagula.

Aliitaka COPRA kuendelea kutoa elimu kwa wakulima nchini ya umuhimu wa kutumia mfumo huo kuuza mazao yao katika maeneo mbalimbali.

Vilevile, aliiomba mamlaka hiyo kutoa elimu kuhusu vifungashio bora vya bidhaa za choroko kwa ajili ya kupeleka kwenye maghala na kupigwa mnada kwa wanunuzi wa zao hilo. Alisema biashara hiyo ya minada itasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima wa zao hilo kupiga hatua kwa maendeleo na kuinuka kiuchumi kupitia kilimo hicho.

Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao na Ubora wa COPRA, Kamwesige Mtembei, alisema katika mnada huo kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kilo 143.113 za choroko zimeuzwa katika maghala ya Dofu, Sotera na Dutwa.

Mkurugenzi wa COPRA, Irene Mlola, alisema mamlaka hiyo imejidhatiti kuhakikisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko inafanyika kwa uwazi na haki.

Irene, alisema vibali vya usafirishaji wa mazao ya dengu, mbaazi, choroko, soya na ufuta vitatolewa kwa wanunuzi waliosajiliwa na kununua mazao hayo kupitia mifumo elekezi ya serikali. Aliwataka wakulima na wanunuzi kutumia fursa za kuwepo wa mamlaka hiyo kunufaika na kilimo cha mazao hayo yanayolimwa katika ukanda huo.

Alisema serikali imewekeza katika sekta ya kilimo, hivyo wakulima wanapaswa kutumia fursa hiyo kukabiliana na umaskini, kujiinua kiuchumi na kutanua wigo wa kilimo cha mazao hayo.

# Madiwani waja juu taka kuzagaa mitaani

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Tarime mkoani Mara, wameutaka uongozi wa halmashauri hiyo kumuwajibisha Mkuu wa Kitengo cha Mazingira kwa tuhuma za uzembe kwa kuacha taka zikizagaa kwenye makazi na kuhatarisha afya za wananchi.

Walitoa rai hiyo katika kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri hiyo kilichofanyika mjini hapa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, madiwani hao walisema kitendo cha taka hizo kuzagaa kwenye baadhi ya mitaa ya halmashauri hiyo kinatokana na uzembe wa mkuu wa kitengo hicho.

Diwani Kata ya Turwa, Chacha Machugu, alidai tatizo hilo linaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa katika halmashauri hiyo na kutaka mkuu wa idara hiyo kuwajibishwa kwa kushindwa kudhibiti uchafu huo.

Machugu, alidai ofisa huyo, ameshindwa kusimamia ukusanyaji taka na kupelekwa Nkende eneo walilotenga kwa ajili ya kutupa takataka.

Aliomba baraza hilo kwa ridhaa ya Mwenyekiti wa halmashauri hiyo kugeuzwa na kuwa kamati ili kujadili suala hilo kwa kirefu na kumwajibisha atakayebainika kuhusika kwa kanuni za halmashauri.

Mkuu wa Wilaya Tarime, Edward Gowele alisema licha ya kuagiza takataka hizo ziondolewa karibu na makazi ya watu, cha kushangaza hazijaondolewa na badala yake anasikia madiwani hao wakiendelea kulalamika.

Gowele, alisema ni vema watumishi wa serikali wakawa wanazingatia maagizo ya viongozi na kuyatekeleza ili kupunguza kero zinazolalamikiwa na wananchi.

"Leo tena natoa maagizo kwa kitengo kinacho husika, sitaki kusikia jambo hilo likijadiliwa tena, pelekeni takataka maeneo rasmi yaliyotengwa," aliagiza.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, alitaka agizo hilo kutekelezwa mara moja kabla baraza hilo halijaridhia kutoa adhabu dhidi ya wahusika.

Kamote, alisema kuwa kuna madai gari la kuzoa taka limehujumiwa na kuharibiwa na kuwalazimu kukodi magari kwa watu binafsi.

Aliagiza uchunguzi ufanyike bila kumuonea mtu aibu na kuchukua hatua kwa watakaobainika kuhusika na hujuma hiyo.




Ukurasa 13



**TANZANIA IKIWA TAYARI NA 'PPP' YAKE...**
**Ajenda ya 'umuhimu wa mitaji binafsi' ilivyotawala Mkutano Nishafi Safi Dar**

Ukurasa 12



## CHIMBUKO SHERIA WATOTO NJITI...

# Waanzilishi wanaharakati; TUGHE, TUCTA zikapokea kijiti, serikali ikamalizia muhuri

- Pilika zilianza 2017, zimejibu wiki iliyopita
- Wadau walidai likizo wiki 36, wamepewa 40

**Na Frank Monyo**

IJUMAA siku ya mwisho mwezi uliopita, Januari 31, gazeti la Nipashe lilichapisha makala inayosomeka "Kinamama kwenye ajira wenye watoto njiti, namna wanavyoteseka kazini wakiwa na vichanga'..."

Makala hiyo ilieleza madhila wanayokutana nayo wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti, kwa kukosa likizo na muda wa kutosha kuwahudumia watoto wao.

Siku moja baada ya kuchapishwa gazeti hili, serikali nayo kupitia Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, liliridhia hoja ya kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa wanawake wanaojifungua watoto njiti.

Hiyo imekuwa ikipigiwa chapuo kwa muda mrefu na wadau mbalimbali wa haki za wafanyakazi. Kulingana na uamuzi huo, likizo ya uzazi itaongezwa kufikia wiki 40 za ujauzito, huku baba wa mtoto njiti akipewa siku saba za mapumziko.

Ni hatua muhimu na juhudi za wadau ikiwamo taasisi ya Doris Mollel, ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakipigania haki hiyo, kwa lengo la kulinda ustawi na afya za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Watoto hao wanahitaji uangalizi wa karibu kutoka kwa wazazi wao ili kuhakikisha ukuaji wao unakua kwa afya njema.



Madaktari wa watoto waliozaliwa njiti katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), katika picha ya pamoja na wazazi wao, katika Maadhimisho ya Siku ya Taifa ya Watoto Njiti. **PICHA: MAKTABA.**

**SAFARI YA HAKI**

Majadiliano kuhusu hoja hiyo, yalianza rasmi mwaka 2017 na mwaka 2018, suala hilo lilipelekwa bungeni kwa mara ya kwanza.

Mnamo Januari 31, 2025, muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi Namba 13 wa Mwaka 2024 uliwasilishwa bungeni na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Awali, akiwasilisha muswada huo uliopendekeza likizo hiyo iende hadi wiki 36, lakini baada ya majadiliano na kamati husika, serikali ilikubaliana kuongeza muda huo hadi kufikia wiki 40. Ni ujumbe wa tabasamu wa 'kuupiga mwingi!'

Kadhalika, likizo ya baba kwa mtoto njiti imeongezwa kutoka siku tatu hadi saba, ili kutoa fursa inayomsaidia mama na mtoto.

**MAREKEBISHO SHERIA AJIRA**

Mbali na suala la likizo ya uzazi, muswada huo umependekeza mabadiliko mengine kadhaa katika Sheria za Ajira nchini. Kifungu kipya cha 34 A kimependekezwa ili kumruhusu mwajiri kumpatia mwajiriwa likizo bila ya malipo isiyozidi siku 30 kwa dharura au majanga yanayoweza kutokea.

Pia, Kifungu cha 14 kinabainisha aina mpya za mikataba ya ajira, ikiwamo ajira ya muda maalum kwa wale wanaojifunza kazi au katika mazingira maalum kama vile misimu ya kilimo au utalii.

Vilevile, Kifungu cha 37 kinazuia mwajiri kuanzisha au kuendelea na shauri la nidhamu dhidi ya mwajiriwa endapo mgogoro huo upo mbele ya Tume ya Usuluhishi na Mahakama ya Kazi.

Lengo la hatua hii ni kuzuia uingiliaji wa mchakato wa kushughulikia migogoro ya ajira.

**LIKIZO WAZAZI WA NJITI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq, alipendekeza serikali kuboresha sheria hiyo zaidi kwa kuzingatia pia haki za akina mama wanaojifungua watoto wenye mahitaji maalum kama vile watoto wenye usonji, vichwa vikubwa, mgongo wazi, mdomo sungura, matundu kwenye moyo, na seli mundu.

Mapendekezo hayo yanalenga kuhakikisha watoto hao wanapata uangalizi wa karibu kutoka kwa wazazi wao kwa muda wa kutosha.

Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete, akawataka wanaume wanaopewa likizo ya wiki moja, kutumia muda huo kuwahu-

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

### TANZANIA IKIWA TAYARI NA 'PPP' MKONONI...

# Ajenda ya 'umuhimu wa mitaji binafsi' ilivyotawala Mkutano Nishafi Safi Dar

• Mkurugenzi Kafulila na namna PPPC inakusanyia mitaji serikali

**Na Salome Kitomari**

AZIMIO la Dar es Salaam la wakuu wa nchi na serikali, kwa ajili ya kutoa nishati ya umeme kwa Waafrika milioni 300 hadi mwaka 2030.

Tayari imeshakubaliwa na kutiwa saini katika kikao cha kati ya Januari 27 hadi 28, mwaka huu na wakuu wa nchi 24 zilizohudhuria Mkutano wa Nishati Safi uliopewa jina 'Mission 300.'

Ulikuwa na lengo la kuhakikisha upatikanaji, uendelevu na manufaa ya kiuchumi kwa wananchi milioni 300 wa Afrika.

Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye katika mjumuiko huo sasa ana wasifu wa kuwa 'kinara wa nishati safi ya kupikia Afrika.'

Pia, akiwa mwenyeji wa mkutano huo, bado ameona fursa kubwa kwenye miradi ya ushirikiano baina ya sekta binafsi na serikali, kwa kutatua changamoto zilizopo kwenye jamii kwa kutumia mitaji ya umma.

Moja ya kipengele katika Azimio hilo ambalo litapelekwa kwenye Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU) ambalo wakuu wa nchi walitia saini na kuridhia kuishirikisha sekta binafsi kwenye miradi ya nishati, ili kutumia mtaji wa umma kutatua changamoto za jamii na kuleta maendeleo.

Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa ni "Kuangaza Afrika kuwa na umeme jumuishi wa kuaminika ambao ni nafuu kwa watu wote" kwani zaidi ya watu milioni 600 wanakosa umeme na nishati safi ya kupikia.

Ili kufikia lengo Namba Saba la Malengo Endelevu ya Nishati kwa Wote mwaka 2030, zinahitajika jitihada za pamoja kupata nishati.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Hamad Yussuf Masauni, kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali, mnamo Januari 28, 2025, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (JNICC), Jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

"Mkataba wa pamoja wa nishati, kutambua umuhimu wa ushirikiano na kutafuta fedha kwa ajili ya ajenda '300' ambapo Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambazo zimejipanga kufikisha nishati kwa watu mil 250 Afrika.

"Lakini, itawezekana ikiwa kutakuwa na ushirikishwaji, kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi na kupata fedha za kuleta mabadiliko kwenye mifumo ya nishati Afrika," anasema.

Wakuu hao wa nchi walisema kwenye Azimio hilo wanatambua kwamba sekta binafsi ina mchango mkubwa katika mnyororo wa uzalishaji na kusambaza na kutengeneza mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ni muhimu sana hasa kwa kuzingatia nishati ni muhimu katika kuchochea maendeleo na kutokomeza umaskini.

Pia, kuna kutoa vivutio kwa sekta binafsi kwa kutengenza mazingira wezeshi ya kisera na mipango kwa kujikita kwenye chambuzi za hasara na faida katika kuandaa sekta ya umeme Afrika.

Siku ya kwanza ya mkutano huo ilitanguliwa na majadiliano ya mawaziri wa nishati na fedha wa nchi hizo za Afrika, ambao walisisitiza dhamira yao ya kukuza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) kwa kuwa na miundo bunifu ya ufadhili katika kupanua wigo wa upatikanaji wa nishati barani Afrika.

Mawaziri hao ambao kwa Tanzania waliwakilishwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakasema mustakabali wa nishati barani Afrika unategemea juhudi za kijasiri zinazochanganya uvumbuzi wa kifedha na mifumo ya kimkakati ya sera.

Tanzania ikafafanua kuwa theluthi moja ya mahitaji yake katika kufadhili mahitaji ya sekta ya nishati, yanaweza kupatikana kutokana na mitaji binafsi.

Hadi sasa nchini kuna sheria, pia sera inayosimamia ubia huo wa PPP, hapo ikitoa ishara bora kwa ajili ya utekelezaji

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais Dk. Samia, akafafanua kwamba katika kufikia malengo ya kujipatia nishati, sekta zote zinapaswa kushughulikia mambo yote yaliyopo kwenye mnyororo wa nishati.

Aanasema, hiyo inafanyika kwa kuweka sera na sheria nzuri za misaada ya kifedha na kiufundi kwa ajili ya ushiriki wa seketa binafsi kuwa na mifumo bora ya kifedha.

PPPC INAVYOIBEBA PPP

Hadi sasa, Tanzania imeshajipanga kutumia fursa ya PPP kwa kuanzisha Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), chini ya mkurugenzi wake, David Kafulila, anayesema wameshasajili miradi 82 iliyoko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa kutumia mitaji ya umma.

Kafulila anasema, ubia ni ndoa ya ushirikiano na si ubinafsishaji kama inavyoelezwa na kwamba miradi ya ubia yote ni mali ya serikali na sekta binafsi inaingiza mtaji kuendeleza.

Aidha, amezitaja sababu za ubia kuwa ni kuvuna mtaji wa sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya serikali badala ya kukopa.

Kafulila anafafanua kwamba, fedha yake serikali inatumia kuwekeza kutekeleza miradi mingine, katika maeneo ambayo sekta binafsi haijaona fursa.

Amezitaja sababu nyingine za uwekezaji kuwa ni, kuvuta mitaji kutoka sekta binafsi,kuvuta tekonolojia ambayo utafiti unaonyesha in sekta binafsi imepiga hatua eneo hilo.

Nyingine anaitaja ni kuongeza ufanisi wa kiutendaji, kwa kuwa sekta binafsi inamudu kusimamia mambo yake kwa ufanisi mkubwa bila urasimu kuliko ambayo serikali ingefanya.

Kwa mujibu wa Kafulila, ni uamuzi unaashiria ufanisi, akitoea mfano kuwa zipo sekta binafsi zinazoajiri wakurugenzi kwa mshahara mkubwa, hivyo kupitia 'PPP', sekta binafsi inaweza kununua mtaalamu mwenye ufanisi mkubwa kwenye utekelezaji wa miradi.

Kafulila anasema, mahitaji ya binadamu yanaongezeka kila siku kuliko uwezo wa serikali yoyote duniani kuyamudu na kwamba, chanzo cha mapato cha serikali ni kodi na mikopo ,hivyo haiwezi kumudu kuyatimiza bila 'PPP'.

"Uzoefu unaonyesha kuwa serikali haiwezi kufikia matarajio kwasababu inategemea kodi na mikopo. Deni la dunia kwa sasa ni dola trilioni 300, huku uchumi ukiwa ni dola trilioni 110 ambayo ni mara tatu ya Uchumi.

"Deni hili ni la serikali, sekta binafsi na kaya...hii inaonesha kuwa hatuwezi kukwepa kushirikiana na sekta binafsi kutekeleza miradi, leo mtu wa Kigoma Vijijini (anakotoka Kafulila) atatamani maisha kama ya mtu wa Kigoma Mjini. Siku akiyapata, atataka ya juu zaidi, hivyo mahitaji ya binadamu yanaongezeka kila siku,"anasema.

"Huwezi kutimiza mahitaji kwa kukopa,lazima ualike sekta binafsi ije na mitaji yake itekeleze,kwa kutumia 'PPP' unatekeleza miradi bila kugusa bajeti na kupunguza shinikizo kwenye vitabu vya serikali.Ilemela mmefanya uamuzi sahihi,"anasema Kafulila.

## WAANZILISHI WANAHARAKATI; TUGHE, TUCTA ZIKAPOKEA KIJITI, SERIKALI IKAMALIZIA MUHURI

Inatoka Uk 11

dumia wake zao na watoto wao, badala ya kushiriki shughuli zisizohusiana na familia.

**AJIRA ZA WAGENI**

Muswada huo pia umeweka masharti mapya kwa wageni wenye vibali vya kazi nchini Tanzania.

Mwekezaji wa kigeni mwenye kibali cha kazi, hatalazimika kupata kibali kingine endapo atakuwa anamiliki hisa katika kampuni tofauti.

Aidha, wakimbizi wenye hadhi stahiki wataendelea kufanya kazi bila kubanwa na ukomo wa muda wa kibali cha kazi.

Pia, kuna kifungu cha muswada huo, kimeweka masharti ya kuzuia urejeshwaji ada ya maombi ya kibali cha kazi, huku Kifungu cha 12, kikirekebishwa kuruhusu maombi ya kuhuisha kibali cha kazi kuwasilishwa angalau miezi miwili, kabla ya kuisha kwa muda wa kibali kilichopo.

**WANAOWAPIGANIA NJITI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Doris Mollel, baada ya bunge na serikali kupitisha mabadiliko ya sheria hiyo, ana ufafanuzi wa sababu za kuanzisha vuguvugu la mabadiliko ya Sheria ya Mwaka 2024 kwa wazazi wanaopata watoto njiti.

Anasema ni kutokana na changamoto nyingi wanazokutana nazo wafanyakazi wanawake wanaojifungua watoto njiti, ikiwamo tatizo la kiafya, msongo wa mawazo na kufutwa kazi kunakotokana na kutumia muda mrefu hospitalini.

Dorice anasema kuwa, tangu mwaka 2017 wamekuwa na shughuli, vikao na harakati mbalimbali za kupambania mabadiliko hayo, wazo likianza mwanzoni mwa mwaka 2017 wakati alipotembelea wodi ya watoto njiti kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, alipoenda kuchangia vifaa tiba hospitalini hapo.

Doris anabainisha, miongoni mwa shughuli zilizofanyika mwanzoni mwa vuguvugu hilo, ni pamoja na vikao zaidi ya 50 vikihusisha wahusika mbalimbali,wakiwamo Umoja wa Wake wa Viongozi Nchini (Millenium Group), Umoja wa Wabunge Wanawake (TWPG).

Pia, kuna wanasheria wa wizara mbalimbali, ,awaziri, Wabunge wanawake, wafanyakazi wanawake, Chama cha Madaktari wa Watoto Wachanga, pamoja na Kamati za kudumu za bunge na maofisa wa wizara mbalimbali serikalini.

Mwaka 2021, Taasisi ya Doris Mollel Foundation ilianzisha Ajenda ya "Mtoto Njiti" na baadae mwaka 2023, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) na Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), nao waliunga mkono jitihada hizo za Doris Mollel Foundation.

Ni suala lililofikisha mwaka jana wakati wa sherehe za siku ya wafanyakazi duniani, Rais Samia Suluhu Hassan akatoa kauli yake ya kwanza hadharani, kupitia kwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akitangaza ujio wa marekebisho ya sheria hiyo ya kazi.

Akimshukuru Rais Dk. Samia, aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri Angellah Kairuki, Doris Mollel anasema kupitia marekebisho hayo ya sheria, Tanzania sasa inakuwa katika nchi chache barani Afrika, zinazounda mazingira jumuishi na bora kwenye kazi, yakizingatia afya ya wazazi wanaopata watoto njiti nchini kote.

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA**

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), nao wametoa pongezi zao kwa serikali, kupitia bunge kuridhia na kupitisha sheria hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa TUGHE, Dk. Jane Madete, anasema ni hatua itakayosaidia kulinda ustawi wa watumishi wanaojifungua watoto njiti nchini, kwani imekua changamoto kwa na ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanawake wanaojifungua watoto njiti.

Anaeleza, wamekuwa wakipitia changamoto zikiwamo za kiafya, hivyo wanahitaji kupata muda wa mwingi wa kupumzika na kumhudumia mtoto, kutoka ngazi ya uangalizi hadi wanaporuhusiwa kutoka hospitalini.

" Pia, wamekuwa kwenye wasiwasi mkubwa wa kupoteza ajira zao, jambo ambalo linaweza kupelekea msongo wa mawazo na hata kuathiri kwa kiasi kikubwa malezi ya mtoto aliyezaliwa" anahitimisha.



## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kweli mgeni njoo mwenyeji apone tumeiona






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

WAKATI tukiwa wadogo vijijini, tulikuwa tukila ugali kwenye visosi na kitoweo kwenye vibakuli au wakati mwingine vyungu au vigae. Yalikuwa maisha ya kawaida kabisa.

Tulizoea hivyo, tukiishi bila wasiwasi na tukisoma kama kawaida ingawa tukilazimika kutembea mwendo fulani mrefu kwenda na kurudi shuleni na tukifanikiwa.

Mathalan katika familia yetu, tulikuwa na kaka yetu aliyekuwa akisoma nje ya kijiji chetu, tukiambiwa anasoma chuo cha ualimu jijini Dar es Salaam, ambako tulisimuliwa kuwa Jiji kubwa lenye kila kitu na kila maisha.

Tukiwa kijijini tulitamba sana kuwa na kaka anayesoma Dar es Salaam, tukiambiwa ndio mji mkuu wa nchi na anakoishi Rais wa nchi, wakati huo akiwa Mwalimu Julius Nyerere.

Tuliona fahari sana kusikia hata kaka yetu anaishi Jiji moja na Rais Nyerere, kwa kweli tulijisikia vizuri sana, tukiamini kuna siku atakuja atuchukue nasi tukalione Jiji hilo lenye sifa lukuki.

Majirani zetu kijijini walijua fika kuwa tulikuwa na mtu tukijimwambafai naye kwa maisha hayo ya kufikirika, utadhani nasi tulikuwa tukiishi Dar es Salaam, kutokana na hisia tulizojivika.

Siku moja nilishangazwa kumsikia mama akitwambia tusilete marafiki zetu kucheza pale nyumbani, kwani alikuwa anatarajia kufanya usafi wa mazingira ndani na nje ya nyumba, hivyo hakutaka bughudha ya michezo ya kitoto.

Tulipomhoji ilikuwaje ghafla hivyo, wakati tulizoea kucheza na watoto wenzetu hapo nyumbani tena tukila pamoja, kama ambavyo tulifanya kwao, kwani enzi hizo mtoto wa mwenzio alikuwa wako kwelikweli.

Baadaye mama alitwambia alikuwa akitarajia ugeni kutoka Dar es Salaam, kumbe kaka alikuwa akija likizo. Tulimwona mama akisafisha hata vikombe na sahani kabatini, ambavyo hatukuwahi kuvitumia tangu vinunuliwe.Ilikuwa mara ya kwanza, kumwona mama akitoa bilauri za glasi kabatini

na kuzisafisha, tayari kutumiwa na mgeni, hatukuwahi kumwona mama akitoa bakuli za udongo na kuzisafisha tayari kwa matumizi ya mgeni.

Hatukutakiwa kabisa kuvisogelea, kwani tungeweza kusababisha ajali na kuvivunja kabla mgeni rasmi hajafika kuvitumia. Na hiyo ilikuwa miongoni mwa sababu za kutukataza kucheza pale nyumbani.

Hakika mama alifanya kazi kubwa ya kuhakikisha mazingira ni safi vyombo ni safi, na hata chumba atakamofikia kaka ni mashalaah.

Tulikatazwa hata kuingiza kitu chumbani mle, bali mama ndiye alijipa ruhusa ya kuingia kusafisha na kufunga mlango.

Tulishangaa kimoyomoyo, huku tukijiuliza sababu ya usafi ule na kwa nini mgeni wetu naye asitumie visonzo kula ugali na vibakuli vya bati au vyungu tu mbona sisi miaka yote hatujadhurika! Kwa wenye chongo nawe vunja lako jicho.

Hakuna aliyeulizwa ili atujibu, kwani kufanya hivyo ilikuwa kuhatarisha

vichwa au makalio yetu kwa makwenzi na viboko mtawalia. Tulisubiri kushuhudia siku mgeni anawasili, pengine ingekuwa ile ya mgeni njoo mwenyeji apone.

Kweli siku ilipowadia, kaka yetu akawasili na mabegi yake na tukampokea kwa bashasha sana, ingawa hatukuruhusiwa pia kugusa mabegi, bali mama tu na ndiye alimkaribisha ndani nasi kubaki nje kusubiri pengine vijizawadi.

Lakini ngoma ilikuwa kwenye kuoga, kwa sababu hatukuwa na huduma ya mabomba, hivyo ilibidi sote tukaoge ziwani hapakuwa na jinsi lazima aizoee hali, bila shaka naye Dar es Salaam alikuwa akienda baharini kuogelea.

Bahati nzuri wala hakuwa na majigambo, alifurahia maisha kama kawaida, nasi tukafaidi kutumia vyombo vya kisasa kwa chakula, ingawa Mungu si

Athumani, tukafaidi pia kula wali na pilau lililoandaliwa mahsusi kwa ajili ya mgeni.

Haya maisha yako sehemu nyingi, kwamba mwenyeji unajinyima raha na starehe mpaka anapokuja mgeni ndipo nawe unaishi kama binadamu, kwani siku zote unakaa umejinyima hata kwa vitu ulivyonavyo ndani. Bila shaka tumezoea hata watoto kuwanunulia chakula na mavazi mazuri siku kuu.

Bila shaka mliona tulipokuwa na Mkutano wa Nishati Dar es Salaam, jinsi Jiji lilivyokuwa safi na wazi kana kwamba halikuwa na wenyeji.

Yawezekana wageni waliokuja kwa siku hizo mbili, waliamini wakazi wa Dar ni wafanyakazi watiifu wasiozurura wakati wa kazi.

Wapo walioamini kuwa kumbe Jiji la Dar haina vurugu za mapikipiki na mabajaji, ni shwari na tulivu wakati wote na ndiyo sababu linaamini

katika nishati safi isiyochafua mazingira. Kwa kifupi waliamini Dar ni Jiji lenye mazingira safi na salama kwa binadamu kuishi!

UCHUMI

# BOSI UNICEF: Tunamuona msichana nchini anavyoendelezwa, tunauona unasaba wake Mama Mongella kwenu

**Na Mary Kadoke**


Wanufaika wa huduma za kielimu wa wasichana mkoani Songwe, katika picha na ugeni wa UNICEF mkoani humo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

TANZANIA hadi sasa inatambuliwa kimataifa kwa sera zake za usawa wa kijinsia, ikipiga hatua kubwa katika kuwawezesha wanawake na wasichana.

Hili lilithibitishwa na Dk. Lauren Rumble, Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa Masuala ya Usawa wa Kijinsia, wakati wa ziara yake hivi karibuni mkoani Songwe, alikotathmini juhudi za Tanzania katika kuwawezesha wasichana balehe.

Ziara yake ilionesha uongozi wa Tanzania na mbinu yake shirikishi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na wa kimataifa.

**HALI YA UONGOZI**

Ziara ya Dk. Lauren ilifanyika wakati muhimu, Tanzania ipo chini ya uongozi wa Rais wa kwanza mwanamke, Dk. Samia Suluhu Hassan, aliyefanya mageuzi makubwa.

Hiyo inatajwa, hata ngazi ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Kama kiongozi wa kwanza Mwanamke wa nchi katika ukanda huu, anafungua milango mipya kwa wanawake na wasichana.

“Tanzania imepiga hatua kubwa katika usawa wa kijinsia. Jambo la kwanza nililogundua ni kuwa, kama wengi wanavyosema.

“Tanzania ni nchi yenye maendeleo makubwa katika masuala ya usawa wa kijinsia, hasa sasa ambapo Rais Dk. Samia ndiye Rais wa kwanza mwanamke nchini Tanzania na Afrika Mashariki,” anasema.

UWEZESHAJI WASICHANA

Pia, kumekuwapo kipaumbele cha UNICEF, katika moja ya maeneo makuu yake nchini kuwawezesha wasichana balehe.

Dk. Lauren anaisifu mbinu shirikishi ya nchi, akisisitiza kuwa juhudi za Tanzania zinajumuisha sekta za elimu, afya, ulinzi wa mtoto na lishe. Ni mkakati mkubwa na muhimu kwa kushughulikia changamoto, ambazo zimekuwa vikwazo kwa maendeleo ya wasichana.

Anaongeza: “Mbinu ya Tanzania kwa ‘usawa wa kijinsia’ imechangia mafanikio yake katika kuboresha maisha ya wasichana.

“UNICEF imekuwa ikishirikiana na serikali ya Tanzania, mashirika ya kiraia (CSOs) na sekta binafsi kuunda mazingira rafiki kwa wasichana, kuhakikisha mahitaji na sauti zao zinasikilizwa.”

**HOJA YA KURUDI SHULE**

UNICEF inataja umuhimu wa Elimu ya Wasichana, kwamba ni hatua muhimu kwa, kupitia mwongozo wake ‘Kurudi Shule’ inayowapa fursa kinamama vijana kurejea shuleni baada ya kujifungua.

Inatajwa hiyo kushughulikia changamoto za kielimu, zinazowakumba wasichana wanaopata ujauzito na kuacha masomo.

Ni mwongozo uliowahi kusitishwa, kiserikali na kurejeshwa tena na Rais Samia, alipoingia katika uongozi mwaka 2021.

Kurudishwa huko, sasa kunatajwa ni hatua kubwa kuelekea usawa wa kijinsia, kwani imewapa wasichana fursa ya kuendelea na elimu yao na kurejesha heshima yao.

Inatajwa kuwaunga mkono kinamama na vijana, serikali ikiwasaidia kukamilisha masomo yao, pia inapunguza unyanyapaa unaohusiana na mimba za utotoni.

Ni hatua inayowawezesha wasichana kurudi shuleni baada ya kujifungua, hivyo kuvunja mzunguko wa umaskini.

**AFYA, ULINZI WA MSICHANA**

Tanzania, hapa inatajwa na UNICEF imepiga hatua kubwa, kushughulikia mahitaji ya afya ya wasichana balehe. Dk. Lauren akisifu upatikanaji wa huduma rafiki kwa vijana.

Hapo anataja vigezo kama vile, chanjo ya HPV inayowakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, ambayo ni miongoni mwa visababishi vikuu vya vifo kwa wanawake duniani.

Pia, kunatajwa huduma za afya, ikiwa ni sehemu ya mkakati mkuu wa Tanzania kuboresha afya ya vijana, ikiwamo utoaji lishe bora na huduma za kinga.

“Mbinu madhubuti ya Tanzania kuhusu afya ya vijana, imehakikisha kuwa wasichana si tu wanakingwa dhidi ya saratani, pia wanasaidiwa kuboresha ustawi wao kwa ujumla,” anasema.

Kwa kushirikiana na UNICEF, Tanzania imeboresha huduma zake za afya, kukidhi mahitaji maalum ya wasichana wanapokua na kuingia katika utu uzima.

**CHANGAMOTO ZINAZOENDELEA**

Licha ya mafanikio makubwa, changamoto bado zipo. Mimba za utotoni na ndoa za utotoni bado ni vikwazo vikubwa kwa usawa wa kijinsia nchini Tanzania.

Kwa kiwango cha mimba za utotoni cha asilimia 22, wasichana bado wanakosa fursa ya elimu na maendeleo wanayohitaji ili kufanikisha maisha yao.

Ndoa za utotoni, ambazo mara nyingi husababisha kuacha shule mapema na fursa chache za maisha, ni changamoto nyingine inayoendelea.

Dk. Lauren anasisitiza kushughulikia changamoto hizo, kunahitaji suluhisho pana, ikiwamo upatikanaji bora wa elimu na huduma za afya.

“Wasichana balehe mara nyingi wanakosa huduma zote wanazohitaji,” anasema kushughulikia pengo hilo, itakuwa muhimu katika kufanikisha usawa wa kijinsia ambao Tanzania inautamani.

UNICEF ikishirikiana kwa karibu na serikali za mitaa na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), inaeleza kuendeleza kukuza sera zinazowalinda wasichana na kuondoa mila hatarishi.

Ni juhudi zinazolenga kuunda mazingira wezeshi kwa wasichana kustawi na kufikia ndoto zao.

**WITO WA UONGOZI**

Dk. Lauren pia anatafakari maendeleo tangu Mkutano wa Beijing wa 1995, uliowekwa kwa mtoto wa kike katika kitovu cha maendeleo ya kimataifa.

Hapo akabainisha kuwa, kuchaguliwa kwa Rais Dk. Samia, ni hatua muhimu katika safari ya kuongeza idadi ya wanawake viongozi Afrika Mashariki.

“Tunahitaji wanawake wengi zaidi katika nafasi za uongozi. Rais mmoja mwanamke haitoshi. Tunahitaji viongozi zaidi kama Mama Samia.”

Aidha, akatoa wito wa uwekezaji zaidi katika kuwawezesha wasichana, hasa kupitia maendeleo ya kiuchumi, elimu ya fedha, na ujenzi wa amani.

Kiongozi huyo wa UNICEF anafafanua matumaini yake kuwa, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Tanzania 2050 itajumuisha mipango ya kuhakikisha kuwa wasichana wanapata nyenzo na fursa za kuchangia katika ukuaji na ustawi wa taifa.

**URITHI WA MONGELLA**

Anataja maendeleo ya Tanzania katika usawa wa kijinsia, pia yanatokana na urithi wa viongozi anaotaja kwa mfano,

Gertrude Mongella, Katibu wa Mkutano wa Beijing wa mwaka1995, uliojadili mustakabali wa maendeleo ya mwanamke duniani, sasa anatajwa alichangia kwa kiasi kikubwa kutetea elimu na uwezeshaji wa wasichana.

UNICEF wanataja juhudi zake zisizochoka, zilisaidia kuingiza ajenda ya mtoto wa kike katika sera za maendeleo ya kitaifa, ikiwamo Tanzania.

Dira ya Mongella haikuwa tu kuhusu elimu bali juu ya kuunda dunia ambapo wasichana wanaweza kufanya maamuzi kuhusu maisha yao ya baadaye.

Kazi yake inaendelea kuhamasisha sera nchini Tanzania, zikihakikisha kuwa wasichana wanapata msaada na fursa wanazohitaji ili kufanikisha maisha yao.

**TANZANIA INABAKI MFANO**

Maendeleo ya Tanzania katika usawa wa kijinsia, sasa UNICEF inaitaja kuwa mfano kwa mataifa mengine.

Kupitia uongozi wa maono, mabadiliko ya sera na ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, Tanzania inajenga mustakabali mzuri kwa wasichana na wanawake wake.

Hata hivyo, changamoto bado zipo, na safari ya kufanikisha usawa kamili wa kijinsia itahitaji juhudi zinazoendelea.

Kwa uongozi wa Rais Dk. Samia na msaada wa washirika wa ndani na wa kimataifa, Tanzania inaendelea kuunda jamii ambapo kila msichana ana nafasi ya kufikia ndoto zake.


Wawakilishi kutoka UNICEF makao makuu na UNICEF Tanzania wakiwa na wasichana balehe, pia wanachama wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto (WCPC) katika Kituo cha Elimu ya Watu Wazima cha Old Vwawa, Mbozi mkoani Songwe.

- ***Makala hii ni yatokanayo na ziara yake nchini, Dk. Lauren Rumble, Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa Masuala ya Usawa wa Kijinsia.***





# Wafanyakazi TRA watakiwa kuacha kukadiria kodi ofisini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAFANYAKAZI wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wametakiwa kuacha kufanya makadirio ya kodi ofisini ili kuondoa malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kiwango ambacho hakiendani na biashara zao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda wakati akizungumza na wafanyabiashara mkoani hapa.

Mwenda, alisema kila mfanyabiashara anatakiwa kulipa kodi kwa usawa kuendana na biashara yake na uwezo wake.

Alisema, watumishi hao wanatakiwa kwenda kuwatembelea wafanyabiashara kuangalia mwenendo wa biashara zao na kuwakadiria.

"Hiki ni kipindi cha makadirio, meneja usikae ofisini nendeni mkawatembelee walipakodi mkaone biashara zao na wakadiriwe kulingana na uwezo wa biashara zao," alisema.

Mwenda, alisema TRA itahakikisha inasimamia usawa ili kila mtu alipe kodi.

Vilevile aliagiza kama wapo wafanyabiashara ambao hawapo kwenye orodha ya walipa kodi waiingizwe ili nawao waanze kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

"Usawa huu wa kulipa kodi uwepo hata kwenye utoaji wa risiti ambazo zitoke si kwa Mkoa wa Singida tu itoke kwenye mikoa yote 33 kwa mtu anapouza au kununua bidhaa," alisema.

Kamishna huyo, alisisitiza watumishi hao kushirikiana vizuri na wafanyabiashara kwa kuwa kila upande unamtegemea mwenzake katika mapato.

**Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni wateja kufungiwa umeme kupitia wakala wa TANESCO bila kupewa stakabadhi, umeme wa wizi na kutolipa ankara za umeme.**

"TRA na wafanyabiashara sio maadui maana sisi hatupo kama nyie (wafanyabiashara) hampo kama sisi, kazi yetu ni kukusanya kodi msipofanya biashara tutakusanya kodi gani?" Alihoji Mwenda.

Alimuagiza Meneja wa TRA wa mkoa huo, Josephat Mwaipaja kuitisha mkutano haraka kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi kwa taasisi na mashirika yasiyo ya serikali ili waelimishwe utaratibu wa jinsi ya kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi.

Vilevile, alimuagiza meneja huyo kuangalia madeni nyuma ya wafanyabiashara ambao wanadaiwa ambao walikuwa wanashindwa kulipa 'return' zao wasamehewe kwa asilimia 50.

"Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) ametuagiza tusifunge biashara za watu badala yake tuwezeshe biashara,"alisema.

Awali Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Mkoa huo, Florian Mallya, aliiomba TRA kuangalia uwezekano kufuta madeni ya nyuma ya miaka mitano iliyopita wanayodaiwa wafanyabiashara.

Mallya, pia aliiomba TRA kupanua wigo wa ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara wote badala ya kuwatoza wale wale wa miaka yote.

Aliitaka mamalaka hiyo kuwatumia viongozi wa vijiji na vitongoji kupata takwimu za wafanyabiashara wote.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA),Yusuph Mwenda (kulia), akizungumza na wafanyabiashara wa Mkoa wa Singida juzi, wakati akisisitiza suala la ulipaji kodi kwa usawa na utoaji wa risiti wakati wa kununua na kuuza bidhaa. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TAKUKURU wafuatilia uunganishaji umeme Bahi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma imefanya chambuzi 14, ikiwemo mfumo wa huduma ya uunganishaji umeme wilayani Bahi ili kubaini mianya ya rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa huo, Victor Swella alisema hayo juzi jijini hapa katika taarifa yake ya utendaji kazi wa taasisi hiyo.

Swella, alisema uchambuzi huo wa mfumo wa huduma ya uunganishaji wa umeme inayotolewa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani humo umelenga kutatua changamoto nyingi zilizobainika. Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni wateja kufungiwa umeme kupitia wakala wa TANESCO bila kupewa stakabadhi, umeme wa wizi na kutolipa ankara za umeme.

Nyingine ni wateja kukosa elimu, maoni na malalamiko.

"Kama TAKUKURU chambuzi zimefanyika ili kusaidia jamii," alisema Swella.

Alisema maazimio yalifanyika ni pamoja na mtumishi wa TANESCO aliyeunganisha umeme kwa mteja kinyemela kuchukuliwa hatua kali kisheria ili kutokomeza vitendo hivyo wilayani humo.

Alisema katika kuboresha utoaji malalamiko,TANESCO Bahi, imeanzisha kundi Sogozi kwa wateja kutoa malalamiko yao na kuwasilishwa sehemu husika ili kupata ufumbuzi.

Chambuzi nyingine zimefanyika katika sekta ya elimu, ardhi, fedha na utawala kubaini malalamiko yalitolewa na wananchi mkoani Dodoma.

Pamoja na mambo mengine, Swella, alisema wamejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele kuzuia rushwa kwa kufanya uchunguzi za tuhuma zilizobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema wamejipanga kuongeza kasi ya ufuatiliaji utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuziba mianya ya rushwa na ufujaji fedha.

# Ofisi ya Waziri Mkuu watakiwa kupendana

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi amewataka watumishi wa ofisi hiyo kutekeleza majukumu yao kwa ushirikiano, upendo, furaha na amani ili kufikia malengo.

Dk. Yonazi, alitoa rai hiyo wakati akizungumza na watumishi ofisi yake kwenye mkutano wake uliofanyika jijini hapa.

Alisema kuna haja kila mtumishi kujifanyia tathimini katika utendaji wake wa kazi, kuzingatia miongozo na kanuni za utumishi wa umma ili kuhakikisha ofisi inapata matokeo iliyoyakusudia kwa ufanisi.

"Ni wakati sahihi kila mmoja kuilinda furaha aliyonayo awapo mahali pa kazi, isingefaa utoke nyumbani huna furaha na ufike eneo la kazi ukose furaha ni vyema kuja eneo la kazi na kuipata furaha mara mbili kwa kuzingatia mazingira yaliyorafiki katika kutekeleza majukumu," alisema Dk. Yonazi

Alimtaka kila mtumishi wa umma kuwa na desturi ya kuheshimu nafasi ya mwingine bila kujali tofauti miongoni mwao.

" Ni vyema kila mtu akajali mwingine na ikumbukwe hakuna mtu mwenye uwezo mdogo wa kufanya kazi, jambo la msingi ni kuhakikisha ule uwezo uliopewa na Mwenyezi Mungu na mafunzo mbalimbali unatumia vizuri na kuhakikisha uleta matunda mazuri na kuleta maendeleo kwa mchi yetu" alisisitiza.

Aliwaeleza watumishi hao kuwa kila mmoja ni kiongozi katika eneo lake la kazi, hivyo abebe dhamana hiyo kwa weledi na ufanisi mkubwa.

"Naomba nisisitize hapa kila mtumishi aliyepo hapa ndiye Katibu Mkuu kwenye eneo lake, kwa kubeba imani ya kwamba ni Katibu Mkuu anapaswa kuwa na nidhamu na bidii katika kazi ikiwa ni pamoja na kuwa mwaminifu," alisema.

Awali Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk. James Kilabuko, aliwaasa watumishi hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi na kuzingatia sheria za utumishi wa umma huku akiwasihi kuimarisha umoja na mshikamano ili kuiletea Serikali maendeleo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya nchini (TUGHE) Tawi la Ofisi hiyo, Numpe Mwambenja, aliwaomba watumishi kuendelea kujitathimini mienendo yao katika utumishi kwa kufanya kazi vizuri na nidhamu.



# Wananchi wachangishana fedha kujenga kivuko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Itezi Mashariki Kata ya Nsalaga jijini hapa, wameamua kuanza kuchanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kivuko baada ya kuvunjika kwa zaidi ya mwaka mmoja

Wakazi hao wanadai kuwa wamekuwa wakipata shida ya mawasiliano na maeneo mengine kipindi cha mvua kutokana na kujaa maji na mengine kuanza kuingia kwenye makazi yao.

Wakizungumza wakati wakipokea mifuko ya saruji iliyotolewa na Taasisi ya Tulia Trust kwa ajili ya ujenzi wa kivuko hicho, wakazi hao, walisema wamekuwa wakishindwa kufanya shughuli za uzalishaji kutokana na hofu ya kuvamiwa na maji hayo.

Mmoja wa wakazi hao, Stella Francis, alisema watoto wamekuwa wakishindwa kuvuka katika eneo hilo kwenda shuleni na kuwalazimu wazazi kuwasindikiza na kuwasubiri wakati wakirejea nyumbani.

"Tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu, lakini tulikuwa hatusikilizwi lakini baada ya kuonyesha juhudi zetu, wadau wengi wameanza kutushika mkono kama ambavyo mnaona Dk. Tulia na Taasisi yake wametuchangia mifuko hii," alisema Stella.

> **"Tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu, lakini tulikuwa hatusikilizwi lakini baada ya kuonyesha juhudi zetu, wadau wengi wameanza kutushika mkono kama ambavyo mnaona ...**

Husna Pangawazi, alisema vyombo vya moto, yakiwemo magari yanayobeba wanafunzi, vilikuwa haviwezi kupita kwenye eneo hilo kutokana na kukwama mara kwa mara na kuhatarisha maisha yao.

"Tuliamua tuanze kuchangishana wenyewe, kila mmoja alikuwa anatoa kile ambacho anacho, mwenye Sh. 1,000, Sh. 2,000 na hata ambaye anazidi hapo tukapata fedha ambazo tulinunulia mawe na tukaanza kujenga," alisema Husna.

Alisema barabara zinazounganisha mtaa wao na maeneo mengine ni mbovu na kuiomba serikali iwasaidie kukarabati ili kurahisisha mawasiliano.

Neema Mkayule, alisema kuna wakati maji yalikuwa mengi na kuvamia makazi yao na kuhatarisha maisha yao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Lameck Daudi, alisema pamoja na kuchangishana fedha, waliamua kuwaomba wadau wawasaidie na kupata vitu mbalimbali.

Daudi, alisema baadhi ya wadau waliwapelekea mchanga, mawe na wengine akiwemo Spika, Dk. Tulia Ackson mifuko 16 ya saruji. Mwakilishi wa Taasisi hiyo, Lugano Mwangosi, alisema walielekezwa na mkurugenzi wao kupeleka mchango huo na wafanyakazi kuchangia nguvu kazi.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda, mkoani Katavi, Nyabise Sabasi, akikagua madaftari ya wanafunzi wa kidato cha sita, ili kujiridhisha ushiriki wao darasani, shuleni hapo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Sekondari ya wasichana kurejesha somo la kilimo

**Na Grace Mwakalinga,** KATAVI

SHULE ya Sekondari ya Wasichana ya Mpanda iliyopo mkoani Katavi, inatarajia kurudisha somo la kilimo kwa lengo la kuwaandaa wanafunzi kwa uzalishaji baada ya kuhitimu masomo yao.

Hatua hiyo inalenga kuunga mkono juhudi za Serikali katika utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 inayolenga kuongeza ujuzi na ufundi kwa wanafunzi ili waweze kujiajiri wanapomaliza masomo .

Ili kufanikisha lengo hilo, uongozi wa shule hiyo umeomba Serikali inapoajiri walimu iwasaidie kuwapatia wa kilimo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Mkuu wa Shule hiyo, Nyabise Sabasi, alisema ombi hilo linatokana na umuhimu wa somo hilo kilimo ili kuwapa wanafunzi ujuzi na kujiajiri kwa baadaye katika Sekta ya Kilimo.

Sabasi, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1985 kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne. Alisema mwaka 2011 shule hiyo ilibadilisha mtaala wake na kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita na kuliondoa somo hilo. Shule hiyo inamiliki ekari 169 zinazotumika kwa kilimo cha mazao mbalimbali, yakiwemo mahindi.

Nyabise, alisema, tangu alipojiunga na shule hiyo mwaka 2008 somo hiyo liliondolewa, kwa sasa anaona umuhimu wa kurudishwa ili kuwapatia wanafunzi ujuzi na utaalam wa kilimo cha kisasa.

"Kwa sasa tuna mwalimu mmoja wa kilimo, lakini tunahitaji zaidi ili kuanzisha tahsusi hii na kuhakikisha wanafunzi wetu wanapata ujuzi wa kutosha," alisema.

Akizungumzia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, ambayo inajikita katika masuala ya ujuzi na ufundi, alisisitiza kuwa shule hiyo inatarajia kuwa vijana wake watakuwa wakulima bora na kuchangia maendeleo ya kilimo nchini.

Kuhusu ufaulu wa wanafunzi, alisema kuwa walimu wa shule hiyo wanafundisha wanafunzi kwa kutumia mbinu zinazowawezesha kufanya vizuri katika mitihani yao.

## Waganga wakuu wa halmashauri waagizwa kujiandaa kibajeti

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

WAGANGA wakuu wa halmashauri za Mkoa wa Njombe wameagizwa kuandaa mpango wa kujitegemea kibajeti wafadhili wa miradi ya sekta ya afya watakapositisha misaada wanayotoa.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka alitoa agizo hilo kwenye Kikao cha Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC) kilichofanyika kwa ajili ya kujadili bajeti ya mkoa ya zaidi ya Shilingi Bilioni 245.4 kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Mtaka, alisema upo umuhimu wa halmashauri kujipanga mapema ili kuhakikisha utoaji wa huduma hauathiriki ikiwa wafadhili wataacha kusaidia miradi mbalimbali.

Aliwaonya waganga hao na wataalamu wa afya wa mkoa huo kuacha tabia ya kutoza fedha wala vifaa tiba wajawazito kwa kuwa huduma inatolewa bure.

"Hii ni aibu kubwa kwa mkoa wetu, sitaki kusikia kuwa kuna mjamzito anatozwa hata senti tano kwa ajili ya gloves, pamba au kifaa chochote cha kujifungua, hili jambo likome mara moja," alisema Mtaka.

Mtaka, alisema serikali imetenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya sekta ya afya, hivyo hakuna sababu ya kuwabebesha mzigo wajawazito wanaojifungua.

Kwa upande mwingine, alitoa rai kwa viongozi wa dini kuendelea kuwahimiza waumini wao kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi.

"Wananchi wanapaswa kuachana na tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa sababu inasababisha vifo visivyo vya lazima na kudhoofisha mshikamano wa jamii na masuala ya sheria waachieni vyombo vya dola," alisema Mtaka.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Frank Mganga, alisema vifaa vya kutolea huduma vinapatikana, hivyo hakuna mwananchi atakayetozwa.

Baraza hilo la ushauri la mkoa huo, limepokea taarifa ya utambulisho wa mradi mpya wa Lishe ya Mwanao yenye lengo la kuimarisha mifumo ya kijamii kutoa huduma za lishe.

Lengo lingine ni kuboresha lishe ya mama na mtoto mkoani hapa ili kutokomeza udumavu.

TANGAZO

MuCoBa Bank PLC

"Kwa Maendeleo Yako"

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-06-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/06/2024 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 31/03/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 344 | 386 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 28 | 9 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,608 | 1,452 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | | |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,969 | 14,221 |
| 12 | Mali nyingine | | |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 3,660 | 3,670 |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | | |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **263** | **304** |
| | | 19,872 | 20,041 |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 12,754 | 12,567 |
| 18 | Amana za Wateja | | |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 49 | 49 |
| 20 | Amana Maalumu | | |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 87 | 143 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | | |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | | |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 283 | 340 |
| 28 | Madeni | 3,052 | 3,368 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | 16,225 | 16,467 |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,647** | **3,573** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | | |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,984) | (5,984) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 121 | 47 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 721 | 721 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | | |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,647 | 3,573 |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | | |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | | |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,130 | 971 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 167 | 167 |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 18.35% | 17.83% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 12.80% | 10.46% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 114.79% | 118.49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70.29% | 70.96% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 90.32% | 90.15% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.49% | -6.15% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.84% | -4.93% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/06/2024 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/06/2023 | Limbikizo lamwaka sasa 30/06/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/06/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 570 | 474 | 1,090 | 964 |
| 2 | Gharama za Riba | (137) | (134) | (231) | (312) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **433** | **340** | **859** | **652** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (7) | (0) | (7) | (198) |
| | | | | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **229** | **223** | **440** | **422** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 229 | 223 | 440 | 422 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | | | - | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(580)** | **(684)** | **(1,170)** | **(1,409)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (266) | (389) | (538) | (780) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | (15) | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (314) | (280) | (632) | (628) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **74** | **(121)** | **121** | **(533)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | (10) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **74** | **(121)** | **121** | **(543)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | | - | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **74** | **(121)** | **121** | **(543)** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | | 55 | 55 | 55 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | | - | - | - |
| 15 | Idadi ya Matawi | | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.37% | -0.57% | 42.73% | -2.51% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 2.04% | -3.50% | 0.74% | -15.45% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 72.68% | 98.06% | 76.50% | 101.68% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 2.70% | 2.00% | 303.14% | 3.07% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/06/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita 31/03/2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/06/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/06/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 74 | 47 | 121 | (534) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 41 | 71 | 112 | 109 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 252 | 598 | 850 | 1,160 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 187 | (823) | (636) | (73) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (113) | (119) | (233) | (202) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 10 | (55) | (45) | (16) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (10) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **450** | **(280)** | **170** | **433** |
| | | | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | - |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | (40) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **-** | **-** | **(40)** |
| | | | | - | - |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (316) | (145) | (461) | (676) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(316)** | **(145)** | **(461)** | **(676)** |
| | | | | - | - |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | - | - |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | - | - |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 134 | (425) | (291) | (283) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,847 | 2,272 | 2,272 | 2,646 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **1,980** | **1,847** | **1,980** | **2,363** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30-06-2024
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2024** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 121 | - | 121 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,862)** | **721** | **3,648** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2023** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,789 | (5,543) | 676 | 3,922 |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (395) | - | (395) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | (45) | 45 | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2024

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Denis Rweyendera .................................. Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | 18/Jan/2024 |
| Kelvin Mushi ............................................. Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | **18/Jan/2024** |
| Saleh S. Abdallah...................................... Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | **18/Jan/2024** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Bakar R Bakar..................... (Imesainiwa) Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | **18/Jan/2024** |
| 2.Prof. Dominicus Kasilo ........................ (Imesainiwa) Mkurugenzi | **18/Jan/2024** |

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Brighter William Mgogosi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0255-0591** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **St. Christina Girls Secondary School** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/22457/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ANJELLA ZEPHANIA MDUMA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 796184** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ DAR/UBU/20403/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ALLEN NELSON MWAMBIPILE** naomba kutangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria yenye namba **TAE422056** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 16/09/2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/21691/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MWAKA MOHAMED KASHUSHU** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 717806** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 21/03/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ DAR/TEM/17056/2025.**

## KUPOTEA KWA LIVING CERTIFICATE



**ABDALLAH MKUMBUKWA** anatangaza kupotea kwa Living certificate, namba mtihani ni **S1486-0044** Kilichotelewa na MURAD **SADDIQ SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/54252/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**IKAMBA ROBERT MSANGA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Toyota hilux pickup yenye namba za usajili **T 619 AAV** Chasses Namba **RN36017751** Engine Namba **18R2030945.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **PHQ/KIL/MOS/2598/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**KEVI OPHIA NGAILO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 193 EBN** AINA YA TVS KING YENYE RANGI NYEUSI KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/1025/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 630 ALU, MC 237 CDV,** na **MC 983 CGG** zote aina ya **KING LION.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/412/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 314 AMD – SAN MOTO, MC 608 CJE – TVS na MC 184 CEW – KING LION.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/414/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 128 CGA**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/416/2025.**

## KUPOTEA KWA BARUA ZA OFA YA KIWANJA

**NICHOLAS AIDAN MBARUKO,** Anatangaza kupotelewa nabarua ya ofa yakiwanja yenye plot no **226,** block a, ilazo north-dodoma city council yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/4920/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU DOTTO MBILIZI FREDRICK** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T931 CMU** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/GEI/GEI/875/2025**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMAIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 2047 YA MWAKA 2025**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA JACKLINE YAHAYA SAFARY.......................MAREHEMU**

**CALVIN DAVID MSUYA................................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 28 Mwezi FEBRUARI, Mwaka 2025.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 31 Mwezi JANUARI Mwaka 2025.

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMAIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 553 YA MWAKA 2025**

**REFERENCE NO 20250108100000553**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA MARIA BENEDICT MBERESERO................MAREHEMU**

**NAZA JOHN MBWAMBO..............................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 10 Mwezi FEBRUARI, Mwaka 2025.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **27 Mwezi JANUARI Mwaka 2025.**

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1985 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RALPH JAMES SALIMU**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARIANE HENRY MAUA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of February, 2025.
Dated at KOROGWE this 31 day of January, 2025.

DISTRICT COURT TANZANIA KOROGWE

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

PRINCIPLE RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT COURT

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Brighter William Mgogosi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0255-0591** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **St. Christina Girls Secondary School** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/22457/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ANJELLA ZEPHANIA MDUMA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 796184** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ DAR/UBU/20403/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ALLEN NELSON MWAMBIPILE** naomba kutangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria yenye namba **TAE422056** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 16/09/2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/21691/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MWAKA MOHAMED KASHUSHU** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 717806** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 21/03/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ DAR/TEM/17056/2025.**

## KUPOTEA KWA LIVING CERTIFICATE



**ABDALLAH MKUMBUKWA** anatangaza kupotea kwa Living certificate, namba mtihani ni **S1486-0044** Kilichotelewa na MURAD **SADDIQ SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/54252/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**IKAMBA ROBERT MSANGA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Toyota hilux pickup yenye namba za usajili **T 619 AAV** Chasses Namba **RN36017751** Engine Namba **18R2030945.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **PHQ/KIL/MOS/2598/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**KEVI OPHIA NGAILO**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 193 EBN** AINA YA TVS KING YENYE RANGI NYEUSI KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/1025/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 630 ALU, MC 237 CDV,** na **MC 983 CGG** zote aina ya **KING LION.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/412/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 314 AMD – SAN MOTO, MC 608 CJE – TVS na MC 184 CEW – KING LION.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/414/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MAWAZO DANIEL KUSSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 128 CGA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIG/KIG/416/2025.**

## KUPOTEA KWA BARUA ZA OFA YA KIWANJA

**NICHOLAS AIDAN MBARUKO,** Anatangaza kupotelewa nabarua ya ofa yakiwanja yenye plot no **226,** block a, ilazo north-dodoma city council yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/4920/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU DOTTO MBILIZI FREDRICK** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T931 CMU** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/GEI/GEI/875/2025**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMAIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 2047 YA MWAKA 2025**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA JACKLINE YAHAYA SAFARY.......................MAREHEMU**

**CALVIN DAVID MSUYA................................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 28 Mwezi FEBRUARI, Mwaka 2025.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 31 Mwezi JANUARI Mwaka 2025.

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMAIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 553 YA MWAKA 2025**

**REFERENCE NO 20250108100000553**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA MARIA BENEDICT MBERESERO................MAREHEMU**

**NAZA JOHN MBWAMBO.............................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 10 Mwezi FEBRUARI, Mwaka 2025.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **27 Mwezi JANUARI Mwaka 2025.**

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1985 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RALPH JAMES SALIMU**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARIANE HENRY MAUA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of February, 2025.

Dated at KOROGWE this 31 day of January, 2025.

RESIDENT MAGISTRATE

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

"Kwa Maendeleo Yako"

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-09-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/06/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 716 | 344 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 94 | 28 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,939 | 1,608 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | | |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,190 | 13,969 |
| 12 | Mali nyingine | | |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 3,590 | 3,660 |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 204 | 263 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **19,733** | **19,872** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | - | - |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 13,370 | 12,754 |
| 18 | Amana za Wateja | | |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 49 | 49 |
| 20 | Amana Maalumu | | |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 75 | 87 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | | |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | | |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 260 | 283 |
| 28 | Madeni | 2,375 | 3,052 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | 16,129 | 16,225 |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,604** | **3,647** |
| | | 8,789 | 8,789 |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | (5,984) | (5,984) |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 78 | 121 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 721 | 721 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | | |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | | |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **3,604** | **3,647** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,191 | 1,130 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 373 | 167 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 18.26% | 18.35% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 14.98% | 12.80% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 103.71% | 114.79% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 66.84% | 70.29% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 90.91% | 90.32% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.83% | 1.49% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.70% | -0.84% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/09/2024 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/09/2023 | Limbikizo lamwaka sasa 30/09/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 665 | 678 | 1,755 | 1,642 |
| 2 | Gharama za Riba | (122) | (150) | (353) | (462) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **543** | **528** | **1,402** | **1,180** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | - | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (199) | 36 | (206) | (161) |
| | | | | - | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **220** | **187** | **660** | **608** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | - | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 220 | 187 | 660 | 608 |
| | 6.3 Gawio | | | - | |
| | 6.4 Mapato Mengine | | | - | |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | (607) | **(696)** | (1,777) | (2,085) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (309) | (371) | (847) | (1,152) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | (20) | - | (60) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (298) | (305) | (930) | (873) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **(43)** | **55** | **78** | **(458)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(43)** | **55** | **78** | **(458)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | | - | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(43)** | **55** | **78** | **(458)** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 43 | 56 | 43 | 55 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | - | - | - | - |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | -0.22% | 23.43% | 0.39% | -2.08% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | -1.19% | 3.04% | 2.15% | -13.40% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 68.59% | 80.50% | 73.60% | 92.64% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 3.41% | 3.31% | 0.49% | -2.56% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/09/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/06/2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/09/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | (43) | 74 | 78 | (478) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | - | |
| | Hasara Katika Mali | 59 | 41 | 171 | 135 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 779 | 252 | 1,629 | 878 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 616 | 187 | (20) | 1,285 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (35) | (113) | (268) | (11) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 70 | 10 | 25 | 42 |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (10) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **1,446** | **450** | 1,616 | **1,840** |
| | | | | - | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | (21) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **-** | - | **(21)** |
| | | | | - | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | - | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (677) | (316) | (1,138) | (11) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(677)** | **(316)** | (1,138) | **(11)** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 769 | 134 | 478 | 1,808 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,980 | 1,847 | 2,272 | 2,363 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **2,749** | **1,980** | **2,749** | **4,171** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30-09-2024
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2024** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **78** | **-** | **78** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,905)** | **721** | **3,605** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2023** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,789 | (5,543) | 676 | 3,922 |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (395) | - | (395) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | (45) | 45 | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2024

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Denis Rweyendera.................................. (Imesainiwa)<br>Meneja Mkuu | | **18/Jan/2024** |
| Kelvin Mushi ..................................... (Imesainiwa)<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | | **18/Jan/2024** |
| Saleh S. Abdallah.................................. (Imesainiwa)<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | **18/Jan/2024** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Bakar R Bakar.....................(Imesainiwa)<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | **18/Jan/2024** |
| 2.Prof. Dominicus Kasilo ........................(Imesainiwa)<br>Mkurugenzi | **18/Jan/2024** |

MuCoBa Bank PLC

"Kwa Maendeleo Yako"

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-12-2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 31/12/2024 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/09/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 276 | 716 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 162 | 94 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 747 | 1,939 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | | |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,349 | 13,190 |
| 12 | Mali nyingine | | |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 3,506 | 3,590 |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | | |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **146** | **204** |
| | | 18,186 | 19,733 |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | | - |
| 18 | Amana za Wateja | 11,838 | 13,370 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 49 | 49 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 95 | 75 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | | |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | | |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 304 | 260 |
| 28 | Madeni | 2,292 | 2,375 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **14,578** | **16,129** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,608** | **3,604** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | | |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,984) | (5,984) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 82 | 78 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 721 | 721 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | | |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | **3,608** | **3,604** |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | | |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,382 | 1,191 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 373 | 373 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | | |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 20.00% | 18.26% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 17.28% | 14.98% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 118.42% | 103.71% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 73.40% | 66.84% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 90.92% | 90.91% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -11.46% | 4.83% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -7.84% | -0.70% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2024 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31/12/2023 | Limbikizo lamwaka sasa 31/12/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 535 | 612 | 2,290 | 2,253 |
| 2 | Gharama za Riba | (126) | (58) | (479) | (520) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **409** | **554** | 1,811 | **1,734** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | - | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | 9 | (206) | (152) |
| | | | | - | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **266** | **239** | 926 | **848** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 247 | 239 | 907 | 848 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | | | - | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(671)** | **(649)** | (2,448) | **(2,771)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (337) | (371) | (1,184) | (1,523) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | (23) | - | (80) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (334) | (254) | (1,264) | (1,168) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **4** | **135** | 82 | **(343)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | (10) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **4** | **135** | 82 | (353) |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4** | **135** | 82 | **(353)** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 43 | 50 | 43 | 50 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | - | 4.14 | - | - |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 4 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.17% | 0.36% | 0.58% | -1.55% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 0.88% | -4.73% | 3.04% | -9.76% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 79.80% | 8.96% | 75.11% | 89.37% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 2.68% | 1.46% | 11.88% | 9.62% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/09/2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31/12/2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 33 | (43) | 111 | (343) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | - | |
| | Hasara Katika Mali | 58 | 59 | 229 | 185 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (159) | 779 | 1,470 | 790 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,581) | 616 | (1,601) | (3,075) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | 84 | (35) | (184) | 71 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 84 | 70 | 109 | 70 |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (10) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **(1,481)** | **1,446** | **135** | **(2,312)** |
| | | | | - | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | (51) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **-** | **-** | **(51)** |
| | | | | - | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | - | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (83) | (677) | (1,221) | (386) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | 850 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(83)** | **(677)** | **(1,221)** | **464** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (1,564) | 769 | (1,086) | (1,899) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,749 | 1,980 | 2,272 | 4,171 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **1,185** | **2,749** | **1,185** | **2,272** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-12-2024

(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 82 | - | 82 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,902)** | **721** | **3,608** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,789 | (5,543) | 676 | 3,922 |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (395) | - | (395) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | (45) | 45 | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,789** | **(5,983)** | **721** | **3,527** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2024

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

**Jina Na Cheo** | **Saini** | **Tarehe**

Denis Rweyendera .................................. (Imesainiwa) **18/Jan/2024**
Kaimu Meneja Mkuu

Kelvin Mushi ..................................... (Imesainiwa) **18/Jan/2024**
Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala

Saleh S. Abdallah................................. (Imesainiwa) **18/Jan/2024**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

**Jina** | **Tarehe**

1. Bakar R Bakar....................(Imesainiwa) **18/Jan/2024**
**Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi**

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA MARTINEZ

ARSENAL iko tayari kuvunja rekodi yao ya uhamisho msimu wa joto kwa dau la pauni milioni 100 kwa kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 27. ***(Fichajesh)***

### SESKO ATAKIWA ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 21, anabaki kuwa namba tisa katika orodha ya wachezaji ambao Arsenal ina uwezekano mkubwa wa kuwasaji katika kipindi cha majira ya joto, huku klabu hiyo ya Bundesliga ikiwa na uwezekano mkubwa wa kumpiga bei katika uhamisho wake. ***(Independent)***

### ARSENAL: TULIMTAKA MORATA

ARSENAL pia ilifanya mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Hispania, Alvaro Morata, mwenye umri wa miaka 32, wiki iliyopita kabla ya kujiunga na Galatasaray kwa usajili wa mkopo. ***(Subscription)***

### CITY, AC MILAN VITANI

KLABU ya Manchester City iko tayari kushindana na Real Madrid kwa ajili ya kumnunua beki wa kushoto wa AC Milan, Theo Hernandez, mwenye umri wa miaka 27, iwapo watamkosa beki wa Juventus na Italia, Andrea Cambiaso (24). ***(TeamTalk)***

### KANE ANUKIA SOKONI

KIPENGELE cha kutolewa katika mkataba wa mshambuliaji wa Bayern Munich na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 31, kitapungua kutoka pauni milioni 67 hadi pauni milioni 54 katika mwaka ujao. ***(BILD)***

### SANTOS AMVUTIA MARESCA

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca, anapanga kumtumia kiungo wa kati wa Brazil, Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 20 ambaye kwa sasa yuko Strasbourg kwa mkopo katika kikosi chake cha kwanza msimu ujao. ***(Fabrizio Romano)***

### GARCIA KUTUA EPL

ARSENAL itatafuta kumsajili mlinda mlango wa Timu ya Taifa ya Hispania, Joan Garcia, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Espanyol msimu wa kiangazi. ***(Subscription)***

### TEL ALITAKIWA CHELSEA

CHELSEA ilishindwa katika jaribio lake la kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Mathys Tel, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Bayern Munich. ***(L'Equipe)***

### MALACIA ALIIKATAA WOLVES

MLINZI wa kushoto wa Manchester United na Uholanzi, Tyrell Malacia, mwenye umri wa miaka 25 angejiunga na Wolves siku ya mwisho ya usajili, lakini akachagua kujiunga na PSV Eindhoven. ***(Voetbal Verslaafd)***

### SHERIA YAIBANA CITY

MMOJA wa wachezaji wanne waliosajiliwa na Manchester City dirisha la Januari atakosa mechi yao ya mchujo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid kwa sababu sheria za Uefa zinaruhusu nyota watatu pekee waliosajiliwa kuongezwa kwenye orodha ya kikosi kabla ya hatua ya mtoano. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR: NIMEFURAHI SANA KUREJEA SANTOS

●●●Mbrazil huyo acheza mechi ya kwanza baada ya miaka 12...

**SAO PAULO, Brazil**

BAADA ya takribani miaka 12 kuzichezea timu mbili bora barani Ulaya na kuelekea Saudi Arabia, Neymar amerejea kucheza soka la kulipwa nchini kwao Brazil.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona na Paris Saint-Germain aliingia kama mchezaji wa akiba mwanzoni mwa kipindi cha pili kwa klabu yake ya utotoni ya Santos katika mechi yake ya Kombe la Campeonato Paulista dhidi ya Botafogo SP, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Vila Belmiro, juzi.

Santos walikuwa wakiongoza mechi hiyo kwa bao 1-0 wakati Neymar alipoingia uwanjani na mchezo ulimazika kwa sare ya 1-1.

„Naipenda Santos. Sina maneno ya kuelezea nilichohisi usiku wa leo (juzi) nilipokanyaga tena kwenye uwanja huu," alisema Neymar baada ya mchezo huo.

Nyota huyo wa Brazil, ambaye alitajwa kuwa nyota wa mchezo huo, alikiri bado hajawa timamu kimwili, lakini alisema alipata hisia chanya katika mechi yake ya kwanza katika kipindi cha miezi mitatu.

„Nahitaji dakika na michezo zaidi. Siko fiti kwa asilimia 100. Sikutarajia kukimbia na kupiga chenga nyingi sana usiku wa leo (juzi). Nadhani nitajisikia vizuri katika michezo minne au mitano," aliongeza.

Neymar, ambaye alitimiza umri wa miaka 33 hapo juzi, alikamilisha uhamisho wa kurejea Santos mnamo Januari 31, mwaka huu na kutia saini mkataba wa miezi sita ambao klabu hiyo ilisema inatumaini kurefusha angalau hadi kwenye Fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2026.

Alishinda mataji sita wakati alipokuwa Santos, iliyoko katika jiji la ufukweni nje ya São Paulo, likiwamo Kombe la Copa Libertadores (Ligi ya mabingwa Amerika Kusini) mwaka 2011.

Neymar, ambaye aliwahi kusifiwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, aliondoka Santos na kwenda Barcelona mwaka 2013 kisha akaweka rekodi ya uhamisho ghali zaidi katika historia ya mchezo huo alipohamia PSG kwa euro milioni 222 mwaka 2017.

Alisajiliwa na Al-Hilal ya Ligi Kuu ya Saudia msimu wa joto wa 2023, lakini akapata jeraha la misuli ya paja miezi kadhaa baada ya kuhama akiichezea Brazil katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia.

Licha ya kuumia kwa Neymar, Al-Hilal bado waliweza kushinda ligi ya Saudia msimu uliopita.

Mkataba wa Mbrazil huyo ulitakiwa kumalizika baada ya michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia itakayochezwa kati ya Juni 15 na Julai 13, mwaka huu nchini Marekani.

Baada ya Al Hilal kukataa kumjumuisha kwenye orodha ya kikosi cha timu hiyo kwa kipindi cha pili cha msimu, na Kocha, Jorge Jesus, alisema hakuna nafasi yake tena kwenye timu hiyo, taarifa za kurejea Santos zilianza kushika kasi kabla ya kurejea kwake rasmi.

# Arteta afunguka wanahitaji nguvu

**LONDON, England**

MIKEL Arteta ametoa wito kwa kikosi chake cha Arsenal kujipanga upya wakati wa mapumziko yao ya mazoezi ya hali ya hewa ya joto huko Dubai na kulenga mwisho wa kushinda kombe msimu huu baada ya kupoteza kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle United juzi.

Washikabunduki hao walifungwa mabao 2-0 huko St James' Park huku mabao ya Jacob Murphy na Anthony Gordon yakiihakikishia timu ya kocha Eddie Howe ushindi wa jumla wa 4-0 na kutinga fainali ya Wembley dhidi ya Liverpool au Tottenham itakayofanyika Machi 16, mwaka huu.

Wakati Newcastle wanaweza kulenga kupata taji la kwanza kubwa katika kipindi cha miaka 56, Arsenal wana siku 10 hadi mchezo wao ujao na jana wakisafiri kwa ndege hadi Dubai baada ya ratiba ngumu ya michezo 12 ndani ya siku 41.

"Tunahitaji kumeza hii, ni ngumu," alisema Arteta.

"Tulikuwa na matarajio mengi. Tulijua ugumu wa kazi kwa sababu ya matokeo tuliyoleta kutoka London, lakini hakuna tunachoweza kufanya kwa sasa.

"Tulichoweza kufanya uwanjani dakika chache zilizopita, sasa tunapaswa kuangalia mbele. Kwanza kabisa, nadhani hili litakuwa chungu. Tukiwa Dubai tunatakiwa kuongeza nguvu na twende tena kwa sababu bado tuna mechi mengi za kucheza."

# Kane awekewa kipengele cha kutolewa

**MUNICH, Ujerumani**

HARRY Kane ana kipengele cha kutolewa katika mkataba wake pale Bayern Munich, chanzo kimeithibitishia ESPN.

Gazeti la Ujerumani la Bild limeripoti mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alikuwa na makubaliano ambayo yangemfanya aondoke katika klabu hiyo msimu huu wa baridi kwa takriban euro milioni 80 na utaanza kutumika tena ifikapo Januari 2026 wakati ada itapungua hadi euro milioni 60.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kifungu hicho kipo, ingawa hakuna maelezo maalum yaliyoainishwa na ilisisitizwa, Kane ana furaha kuwa Bayern na hana nia ya kuondoka kwenye timu ya Bundesliga hivi karibuni.

Kane aliondoka Tottenham na kujiunga na Bayern Munich kwa mkataba wa thamani ya pauni milini 100 hapo Agosti mwaka, 2023.

Kama sehemu ya makubaliano hayo, Spurs wana chaguo la kwanza kwa Kane lakini bado wangehitaji kuamsha kipengele hicho au kujadiliana kuhusu bei na Bayern.

Inafungua milango ya uwezekano wa kurejea Uingereza siku moja huku Spurs, Chelsea na Manchester United zikiwa miongoni mwa klabu zilizokuwa tayari kumsajili mshambuliaji huyo mwezi uliopita na huenda ikawa hivyo tena msimu wa joto.

Arsenal pia walikuwa na nia ya kumsajili fowadi huyo, lakini kutokana na upinzani wa London Kaskazini na Spurs, uhamisho wa Kane haungewezekana sana ingawa mchezaji mwenyewe alikuwa shabiki wa washikabunduki hao utotoni kwake.

Kane pia amebakiza mabao 47 kuifikia rekodi ya muda wote ya Alan Shearer ya kufunga magoli 260 kwenye Ligi Kuu England.





# ANCELOTTI AWASIFIA CHIPUKIZI MADRID IKITINGA NUSU FAINALI

**MADRID, Hispania**

KOCHA Carlo Ancelotti aliwasifu vijana chipukizi wa Real Madrid baada ya kuisaidia timu hiyo kushinda mabao 3-2 dhidi ya Leganés, huku Gonzalo García mwenye umri wa miaka 20, akifunga goli la ushindi dakika ya 93 katika mechi ya robo fainali ya Copa del Rey iliyochezwa juzi.

Kikosi kilichobadilika sana cha Madrid, ambacho kilijumuisha walinzi chipukizi Raúl Asencio (21), na Jacobo Ramón (20), pamoja na washambuliaji,Arda Guler (19) na Endrick (18).

Garcia, ambaye amefunga mabao 19 ya ligi katika timu ya akiba ya Madrid Castilla msimu huu, halafu akatoka kwenye benchi na kufunga bao la ushindi akiunganisha krosi ya Brahim Diaz, aliwahakikishia Madrid nafasi ya kutinga nusu fainali.

"Ulikuwa mchezo wa ushindani. Tuliteseka nyuma. Jacobo alikuwa na wasiwasi kidogo mwanzoni, na kisha akaanza kurekebisha mambo. Gonzalo yuko katika hali nzuri kwa Castilla. Inabidi tufurahie kile vijana walichofanya," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Wanaweza kufanya makosa, lakini walichangia timu. Tunawahitaji, ni wakati mgumu. Tunapaswa kupitia kwa michezo kama ya leo, ambapo tuliteseka."

Tatizo la majeraha ya safu ya ulinzi limeiacha Madrid bila mabeki wao watatu wa kati (Éder Militão, Antonio Rudiger na David Alaba), katika hatua muhimu ya msimu huu.

Madrid itawakaribisha wapinzani wao Atletico Madrid kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu katika mechi ya LaLiga itakayochezwa kesho kabla ya kuzuru Manchester City katika mechi ya mkondo wa kwanza wa raundi ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

HABARI MICHEZO

# MZIZE AKIPOTEZEA KIATU, AWAZA UBINGWA WA NNE

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Clement Mzize, amesema mabao anayoyafunga ni kwa ajili ya kuisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya nne mfululizo na kamwe hafikirii tuzo ya mfungaji bora.

Juzi, Mzize alifunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 6-1 dhidi ya Kengold FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na kufikisha mabao tisa.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Mzize anayewindwa na timu mbalimbali a nje ya Tanzania, alisema kama wachezaji wanajituma uwanjani kuhakikisha wanaisaidia timu yao kutetea ubingwa.

„Kikubwa ni ubingwa kwa timu, ligi ni ngumu na kila mchezaji anapambana kuhakikisha malengo ya klabu yanatimia, tumeingia mzunguko wa pili, mzunguko wa lala salama, kila mechi ni fainali kwetu kwa sababu tunataka kuona mwisho wa msimu timu inatetea ubingwa," alisema Mzize.

Aidha, mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa (Twiga Stars), alisema suala la tuzo binafsi kwake ni jambo la pili baada ya ubingwa kutua kwa Yanga.

„Nafunga kuisaidia timu kutwaa ubingwa, suala la mfungaji bora nadhani litatokea lenyewe, mimi binafsi lengo ni kusaidia timu kutetea ubingwa tunaoushikilia," Mzize aliongeza.

Tangu mwaka jana nyota huyo amekuwa akihusishwa na baadhi ya klabu za Afrika Magharibi wakihitaji huduma yake jambo ambalo Yanga bado haijatoa baraka ya kuondoka kwa sasa licha ya ofa nono zilizowasilishwa.

Mzize, anatajwa kutakiwa na CR Belouizdad na MC Alger zote za Algeria pamoja na Kaizer Chief inayoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini, ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa Yanga, Nasreddine Nabi.




Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (jezi ya kijani), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa KenGold, Komanje Sandale, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga ilipata ushindi wa mabao 6-1. **PICHA: MTANDAO**

# Alliance Girls, Fountain dimbani

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kumaliza maombolezo ya msiba wa aliyekuwa mmiliki wa Taasisi ya Alliance, marehemu, James Bwire, kikosi cha Alliance Girls kinatarajia kuikaribisha Fountain Gate Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Nchini itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Alliance Girls yenye pointi 11 iko katika nafasi ya tano ikifuatiwa na Fountain Gate Princess yenye pointi 10.

Milembe John, mshambuliaji wa timu hiyo mwenye mabao matatu msimu huu, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vyema na wako tayari kwa mechi hiyo.

„Tumetoka katika msiba mkubwa, lakini kitimu tuko tayari kwa mchezo, tunaamini tutapambana ili kupata ushindi na kuendelea na safari yetu ya kufikia malengo," alisema mshambuliaji huyo.

Vinara wa ligi hiyo ni mabingwa watetezi, Simba Queens yenye pointi 34 wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 29 lakini ikiwa na mchezo mmoja mkononi.

Bunda Queens kutoka mkoani Mara yenye pointi tisa sawa na Gets Program ya jijini, Dodoma na Mlandizi Queens yenye pointi moja zinaburuza mkia katika ligi hiyo ya juu kwa wanawake hapa Tanzania Bara.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itasimama kwa muda wa wiki tatu ili kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Twiga Stars), ambayo inajiandaa kuikaribisha Equatorial Guinea katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON), itakayochezwa Februari 20, mwaka huu hapa jijini.

## Camara bado chache kumkamata Matampi

**Na Adam Fungamwango**

KABLA ya mchezo wa jana kati ya Simba dhidi ya Fountain Gate, golikipa wa Wekundu wa Msimbazi, Moussa Camara, alikuwa amebakisha mechi mbili za kusimama langoni bila kuruhu bao ili kumfikia kipa bora wa msimu uliopita, Ley Matampi, aliyekuwa akiichezea Coastal Union.

Matamp alibeba tuzo ya Kipa Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024, akiwa na ‚clean sheets' 15.

Mechi ya Jumapili iliyopita dhidi ya Tabora United ambayo Simba ilishinda mabao 3-0, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora, aliyotoka bila kuruhusu wavu wake kuguswa, ilimfanya kufikisha ‚clean sheets' ya 13.

Nafasi ya pili katika makipa ambao wamelinda vyema vyavu zao inashikiliwa na Djigui Diarra wa Yanga ambaye juzi aliruhusu bao la jioni walipocheza dhidi ya KenGold FC kutoka Mbeya.

Camara, raia wa Guinea, aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu akitokea, Horoya FC, amekuwa kwenye kiwango bora kabisa ikiwa ni mara kwanza akicheza Ligi Kuu ya Tanzania, akiwa amekaa langoni mara zote 16 ambazo timu yake imeshuka dimbani.

Idadi kubwa ya michezo iliyosalia ndiyo inayotajwa huenda ataendelea kung'ara zaidi kwenye msimu huu.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la michezo Nipashe, Camara ameruhusu mabao katika michezo mitatu tu kati ya 16 ambayo amekaa langoni.

Alifanya hivyo Oktoba 4, mwaka jana, aliporuhusu mabao mawili, Simba ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal, Union, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam na Oktoba 19, mwaka jana, timu yake ikipata kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Mechi nyingine ilikuwa Desemba 21, mwaka jana, aliporuhusu mabao mawili dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera, Simba ikishinda magoli 5-2.

Ubora wa Matampi, uliifanya Coastal Union kumaliza katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kupata tiketi ya kushiriki katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Patrick Munthary, Mtanzania anayeichezea Mashujaa FC, pia amesimama langoni katika mechi nane bila kuruhusu bao akifuatiwa na Metacha Mnara wa Singida Black Stars mwenye ‚clean sheets' saba huku Mohamed Mustafa wa Azam FC, raia wa Sudan, akiwa nazo sita.



Camara

Michezo
Ijumaa Februari 7, 2025
Nipashe

## Neymar: Nimefurahi sana kurejea Santos

UKURASA 21





Mshambuliaji wa Simba, Elly Mpanzu (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Fountain Gate FC, Shaaban Pandu, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani, Manyara jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Chasambi aigharimu Simba

## ●●●Makosa yake yawanyima pointi tatu Msimbazi, yabakia nafasi ya pili...

**Na Faustine Feliciane**

MAKOSA yaliyofanywa na winga, Ladaki Chasambi dakika ya 75 kwa kurudisha vibaya mpira kwa golikipa, Mussa Camara, yameifanya Simba kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji Fountain Gate katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani, Manyara jana.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kufikisha pointi 44 na kuwaacha mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 45 kibindoni wakitawala kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kila moja ikicheza mechi 17.

Simba walikuwa wa kwanza kupata bao kupitia kwa Leonel Ateba ambaye alipokea pasi safi ya Chasambi ndani ya eneo la 18 na kufunga goli la kuongoza dakika ya 57 kufuatia mpira wa adhabu ndogo ulioanzishwa haraka na Jean Charles Ahoua.

Bao hilo lilimfanya mshambuliaji huyo raia wa Cameroon, Ateba, kufikisha mabao nane msimu huu.

Hata hivyo, Chasambi aliwarudisha mchezoni Fountain Gate baada ya kujifunga kwa mpira mrefu aliourudisha golini huku Camara akishindwa kuokoa hatari hiyo na kuzama nyavuni.

Baada ya bao hilo, wachezaji wa Fountain Gate wakaanza kucheza nyuma ya mpira huku wakifanya mashambulizi ya kushtukiza ambayo hata hivyo hakuna shambulizi lolote lililozaa bao.

Simba waliendelea kulishambulia lango la Fountain Gate lakini umakini mdogo wa washambuliaji uliwanyima kupata mabao kwa nyakati tofauti tofauti ambapo dakika za 47 na 50, Ellie Mpanzu, alipoteza nafasi ya kuipatia timu yake magoli.

Fountain Gate walipata pigo baada ya golikipa wake, John Noble, kuonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyozaa kadi nyekundu dakika ya 81 kufuatia kile kilichotafsiriwa na mwamuzi, Abel William, alikuwa anapoteza muda kwa makusudi.

Noble alionyeshwa kadi nyekundu kipindi ambacho timu yake ilikuwa imemaliza idadi ya wachezaji wanaotakiwa kubadilishwa na kulazimu mchezaji mmoja wa ndani kusimama langoni.

Hata hivyo, mapema Simba iliyoanza kwa kasi dakika ya 11 kupitia beki wake, Mohamed Hussein ,Zimbwe Junior' alifunga bao ambalo lilikataliwa kwa tafsiri mfungaji huyo alikuwa ameotea.

Dakika ya 25, Ahoua, alikaribia kufunga lakini shuti lake kali lilidakwa na Noble kabla ya Che Malobe Fondoh kumjaribu tena golikipa huyo kwa mpira wa kichwa ambao ulitoka nje kidogo ya lango.

Kipindi cha pili Simba ilifanya mabadiliko kwa kuwatoa Ahoua, Chasambi, Ngoma na Hussein na nafasi zao kuchukuliwa na Debora Fernandez, Mukwala, Joshua Mutale na Orkajepha Nouma, mabadiliko ambayo licha ya kuongeza kasi ya kushambulia lakini hayakubadilisha matokeo.

Wakati huo huo katika mechi ya mapema mchana Pamba Jiji kutoka Mwanza ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji.

Matokeo hayo yanaifanya Pamba Jiji kufikisha pointi 15 na kubakia pale pale kwenye nafasi ya 14 kutokana na Tanzania Prisons kupata ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Mashujaa FC na hivyo kufikisha pointi 17.

## Yanga yamzawadia Ramovic ushindi 6G

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kutokuwepo nchini, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ametajwa kushiriki maandalizi ya timu hiyo iliyopata ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya KenGold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Abdihamid Moallin, aliliambia gazeti hili ushindi huo ameupeleka kwa Ramovic, ambaye ameachana na klabu hiyo, Jumanne iliyopita na kujiunga na CR Belouizdad ya Algeria.

Moallin alisema hauwezi kuutengenisha ushindi huo na Ramovic kwa sababu walikuwa wote hadi dakika ya mwisho katika maandalizi.

"Kwanza niwapongeze wachezaji wangu wamefanya kazi kubwa sana, ushindi huu wa mabao sita naupeleka kwa kocha mwenzangu, Ramovic, huwezi kumtenganisha na mafanikio haya, tulifanya naye kazi kubwa katika maandalizi ya mchezo huu, kutengeneza mfumo na kuwasoma wapinzani wetu, kwa hiyo hizi pointi tatu na ushindi huu na yeye pia anahusika ameingia katika rekodi hii. Kwa maana hiyo namzawadia yeye," alisema Moallin.

Aliongeza matokeo ya ushindi mnono yametokana na kufanyia kazi mapungufu waliyobaini katika mechi iliyotangulia dhidi ya Kagera Sugar.

"Tulipoteza nafasi nyingi katika mchezo wetu dhidi ya Kagera Sugar hasa kipindi cha kwanza, tukapata bao moja tu, lakini katika mchezo huu ,tumeua' mechi mapema, tumefunga mabao manne kipindi cha kwanza, hii inaonyesha wachezaji wangu wamekifanyia kazi kile tunachowaelekeza pamoja na mapungufu yaliyojitokeza," alisema kocha huyo.

Aliongeza wataendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanashinda mechi nyingine zinazofuata za ligi hiyo.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, alitaja sababu kadhaa zilizofanya kufungwa idadi hiyo ya mabao, ikiwa ni kichapo kikubwa zaidi kukipata kwa timu yao msimu huu.

"Tumefungwa mabao manne kipindi cha kwanza kwa sababu ya uzembe wa mabeki wangu, ukitizama kuna mabeki ambao niliwategemea watacheza niliowasajili dirisha dogo la usajili lakini hawapo, Steven Duah na Kelvin Yondani na wengine hawajacheza kwa sababu wana kadi za njano. Wapo pia baadhi ya wachezaji ambao vibali vyao havijakamilika, natumaini mechi inayofuata kila kitu kitakuwa tayari," alisema Kapilima.

Alisema kuwa bado hawajakata tamaa ya

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042